

ALAMA YA MNYAMA

 Sasa, kesho usiku...Daima tunaonyesha jambo moja, Bwana Yesu Kristo, ni hivyo tu, na lo lote ambalo ni mapenzi Yake ya Kiungu kwetu kufanya. Lakini kama ni mapenzi Yake ya Kiungu kesho usiku, juu ya *Muhuri Ya Mungu*, tutazungumzia, kama Bwana akipenda.

² Basi usiku wa leo, tukitoa, kama Yeye... ikiwa ni majaliwa Yake kwetu kufanya jambo hilo, ama majaliwa yetu kumfanyia Yeye, hasa, usiku wa leo, tunataka kuzungumza juu ya moja ya masomo yaliyo muhimu sana ya majira haya: *Alama Ya Mnyama*.

³ Basi jana usiku tulikuwa katika nyakati za kanisa, *Nyakati Saba za Kanisa*. Na kuanzia Wakati wa Kanisa la Efeso, la Efeso; ndipo tulimalizia na Wakati wa Kanisa la Laodikia, ule wakati wa mwisho wa kanisa. Basi Bwana na aongeze baraka zake sasa kwa Neno tunapozungumza.

⁴ Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo wa maombi, kabla tu hatujalifungua Neno hili la Kiungu.

⁵ Baba Mwema wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya majaliwa haya tuliyo nayo usiku wa leo, kuwa hai, na kuwa hapa duniani, usiku wa leo, na kuwa na afya na nguvu, na tunaweza kuketi jengoni, ambapo Neno la Mungu linasomwa.

⁶ Nasi tunaomba, Ee Mkombozi mbarikiwa, kwa kuwa u Mkombozi aliye wa Jamaa yetu wa Karibu Ambaye ametuosha kwa Damu Yake, na kutusafisha na dhambi, na sasa unatukabidhi kwa Baba, bila kosa, katika Kristo Yesu; naomba Wewe uje, usiku wa leo, na kuchukua Neno na kulifungulia mioyo yetu. Jalia Roho Mtakatifu achukue Neno linapofundishwa, na jalia liende moja kwa moja hata kwenye lengo lake, kwenye kila moyo, moyo wangu na moyo wa wasikilizaji. Kadiri tulivyo na haja Nalo, Baba, na jalia litolewe. Naomba mtu ye yote asiudhiwe na Neno. Pia, Baba, kama wakati wo wote ningetamka kitu ambacho kingekuwa kinyume cha uongozi Wako, naomba Roho Mtakatifu aufunge mdomo wangu. Nina shauku tu ya kujua lililo Kweli, ndipo nikatembee mle.

⁷ Tubariki pamoja sasa, tusamehe dhambi zetu, kwa kuwa tunapokusanyika katika nyumba hii ya ibada. Pia jalia dhambi zetu ziwe chini ya Damu, na roho zetu ziwekwe katika hali ifaayo ya ibada wakati huu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁸ Sasa, nilikuwa tu ninawaza, kipande hiki kidogo cha karatasi hapa, nilikuwa nimeandika Maandiko kadha ku... ya

kurejea, kusoma, kwanza. Na sasa ninapokuja hapa, inaonekana kama sitaki kusoma yo yote yake. Hivyo ndivyo ilivyo kwa kawaida; mafungu manne matano ya kuanzia.

⁹ Bali nataka kusoma ama kusema jambo hili kwanza, ya kwamba, katika kunena, kamwe siwazii. Mwajua, labda, kama tu. . . Sijapanga la kusema zaidi ya mlivyofanya, mnaona, hata kidogo. Ninamngojea tu Yeye. Na kadiri ninavyoliona, ninanyosha tu mkono na kulichukua, nikawapa. Halafu wakati mwingine linaweza kusikika ni kali kidogo, wakati mwingine, bali ni jinsi tu ninavyolipokea. Kwa hiyo hivyo—hivyo ndivyo tu ninavyoweza kulitoa.

¹⁰ Naam, katika hili, hebu. . . niseme tena usiku wa leo. Hili halielekezwi kwa mtu ye yote binafsi wala dini ya mtu ye yote, unaona, sivyo kabisa. Hatuamini katika jambo hilo. Tunaamini ya kwamba sisi ni Wamarekani wa kweli kabisa, ya kwamba kila mtu anaweza kuwa na majaliwa ya kumwabudu Mungu kulingana na mwongozo wa dhamira Yake mwenyewe. Nasi tunataka jambo hilo liwe hivyo daima. Lakini, katika kila kanisa, tuna fundisho.

¹¹ Mara nyingi, katika mashirika, madhehebu, wana kanuni ya imani. Nao wanadumu katika kanuni hiyo ya imani, “Hii ndiyo kanuni yetu ya imani.” Haidhuru mhudumu anawazia jambo gani, hana budi kufundisha hio kanuni ya imani, kwa maana yeye yumo katika hayo madhehebu.

¹² Basi humu ndani, hatuna kanuni ya imani ila Kristo, huyo ndiye kanuni ya imani; na hakuna sheria ila upendo; hatuna kitabu ila Biblia. Naye Kristo ndiye Kichwa; nayo Biblia ndiyo kitabu chetu cha mafundisho; dunia ndiyo uwanja wangu. Kwa hiyo napenda—napenda kuhubiri tu jinsi ninavyojisikia ninaongozwa kuhubiri, na jinsi tu ninavyoliona.

¹³ Halafu katika wakati huu, katika kunena hasa juu ya sehemu hii inayoparuzi, ngumu, na inayokata ya Injili, lakini, mwajua, hii ndiyo nyumba ya hukumu. “Hukumu huanza katika” (wapi?) “nyumba ya Mungu.” Sawa. Hapa ndipo hukumu inapoanza. Halafu kuna. . . Kama ungeenda hapa mahakamani, nawe ilikuwa uwe na kesi, wao wana kitabu cha sheria pale, hawana budi kusoma sheria hii, kuona ulichohukumiwa. Basi hivyo ndiyo ilivyo katika nyumba ya Mungu, hatuna budi kuitoa kwenye Neno la Mungu.

¹⁴ Basi sasa, mara nyingi, katika vitu hivi, ili mwe na hakika mnalipata hili sasa, ya kwamba, huenda nimekosea. Tafsiri yangu ingeweza kuwa na makosa. Bali mimi hujaribu kulisoma Hilo kwa makini sana, na kusema tu linavyosema. Kudumu tu moja kwa moja na Maandiko, kile yanachosema kitemwe.

¹⁵ Basi sasa ni vibaya tu zaidi, ama. . . Labda si mapenzi ya Bwana, na labda ni mapenzi Yake, sijui, ya kwamba, ningetaka kuwa na juma baada ya juma katika Kitabu hiki, kudumu

tu moja kwa moja hapa na kuliangalia likiungana moja kwa moja huko nyuma katika Danieli, halafu Danieli na Ufunuo, na kuliunganisha na manabii.

¹⁶ Basi Neno lote la Mungu limefunganishwa pamoja kabisa. Vitabu sitini na sita, vilivyoandikwa na watu kadha, walioachana kwa mamia ya miaka, wala hakuna kimoja kinachohitilafiana na kingine, hakuna hata kimoja. Kila kimoja cha hivyo ni kikamilifu. Hakuna kitabu cho chote kilichowahi kuandikwa kama Hicho, ulimwenguni kote.

¹⁷ Wao wamekuwa, kwa miaka elfu mbili, wakijaribu kubadilisha Sala ya Bwana. Kuingiza neno moja Kwake, ama kuondoka moja Kwake, kulifanya liwe bora zaidi. Huwezi kufanya jambo hilo kamwe. Loo, ni kikamilifu. Ni Neno la Mungu.

¹⁸ Nami ninaamini Bi—Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa. Kila Neno Lake limevuvuwa. Siamini *hili* tu halijavuviwa, na *hili* limevuvuwa, na *lile* limevuvuwa. Ninaamini lote limevuvuwa. Aidha lote ni kweli ama lote si kweli; basi iwapo lote limechanganyikana, basi hatujui la kufanya. Bali Hilo, kwa kila sehemu, ni Kweli. Niko tayari kuyotoa maisha yangu wakati wo wote kwa kile kilicho BWANA ASEMA HIVI hapa.

¹⁹ Naam, sasa wao wana siku hizi chache usiku. Na, jambo lingine, tutakuwa na ibada ya Jumamosi usiku, ikiendelea vile vile hasa, juu ya kuwa. . .

²⁰ Jamaa fulani wa kanisa walisema wao wange-...kwamba ni pachafu, kuja kanisani Jumapili asubuhi, ambapo baadhi yao walisema wangebaki Jumamosi usiku, baada ya ibada, na kusaidia kulisafisha kanisa ili kwamba haitawabidi hao watu kuja Jumapili asubuhi, ama wa-...ama haitawabidi kufanya kazi Jumapili, ku—kutayarisha kanisa. Hatunini hii. . . Tunataka. . . Mimi ni Mwanasabato, bali napenda kuiheshimu i—ibada hiyo vizuri niwezavyo.

²¹ Basi sasa, halafu, nafikiri nitatangaza kesho usiku, labda, Bwana akipenda, tutakachozungumzia Jumamosi usiku.

²² Naam, usiku huu ni: *Alama Ya Mnyama*. Halafu kesho usiku: *Muhuri Ya Mungu*. Hayo ndiyo mawili ya. . .nadhani, masomo yaliyo muhimu sana kuzungumziwa katika siku hii, kwa kuwa kweli ninaamini ya kwamba tunaishi katika wakati wa hii hukumu ya uchunguzi ya Mungu. Ninaamini tuko moja kwa moja katika siku hiyo. Nasi hatutaki kuwa wapinduzi. Hatutaki kuwa washupavu wa dini. Tunataka kuliendea kwa akili timamu tu kama Biblia itakavyolinena hapa; na Hiyo ni kamilifu, bila shaka.

²³ Basi sasa katika kufanya jambo hili, tunawasikia watu wengi sana, leo, wakizungumza juu ya alama ya mnyama. Mmesikia jambo hili kwa muda mrefu, “Ni kitu gani? Ni nani anayefanya jambo hilo? Ni wapi? Ni nani atakayeipata? Na kama wakiipata,

i—itawafanya nini kwao? Ati nini? Nani anaifanya? Ingeweza kukudhuru? Hivi kuna—hivi kuna madhara yo yote kwake?”

²⁴ Vema, sasa, hilo ndilo tu—tunalotaka tuone kutoka kwa Neno la Mungu, jambo la kwanza, “Iwapo kuna alama ya mnyama iliyonenwa katika Biblia?” Halafu jambo jingine, “Itahusu wakati gani? Na ni watu gani watakaokuwa nayo? Nawe ungefanya nini? Hivi ungeweza kuipata wala usijue?” Na kadhalika, hayo, maswali hayo tu namna hiyo. Kwa hiyo, nijuavyo mimi, ni ya kwamba—ya kwamba jambo hili lingekuwa moja la masomo yaliyo mhimu sana ninayoweza kuwazia katika Biblia, *Alama Ya Mnyama*, na *Muhuri Ya Mungu*.

²⁵ Naam, kwanza, ninalo Andiko hapa kuonyesha kama... ama ndiyo kwanza niandike, ili kwamba tu ningeweza kulifungua, na hilo ni Mtakatifu... Kwanza, hebu tu tuone alama ya mnyama ni nini, kisha, “Je! ni hatari kupata alama hii? Ni hatari?” Sasa katika Ufunuo, sura ya 14 na aya ya 9, ni ujumbe wa yule malaika wa tatu. Naam, mwanachuoni ye yote wa Biblia...

²⁶ Ninamwona Ndugu Stanley hapa, na wahudumu wawili watatu walioko hapa. Na jana jioni kulikuwako na ndugu wengine hapa kutoka seminari ya Batisti huko Louisville, na labda kuna wengine usiku huu. Sijui. Na labda kuna Methodisti, Batisti, Katoliki, na huenda kukawa na Orthodoksi ya Kiyahudi. Sijui. Lakini si...

²⁷ Hii si kuiudhi dhamira ya mtu ye yote; la hashu. Na ni kwa nini hii tu... Jinsi tu Biblia ilivyoandikwa, kuisoma, na kukuacha uangalie, wewe binafsi. Basi hebu tuikaribie kwa akili timamu tujuavyo sisi, katika hicho cha Mungu, tukijua ya kwamba Yeye atatu hukumu kwa ajili ya maneno yetu. Maneno yetu aidha yatatubariki sisi ama kutuhukumu kwenye ile Siku ya Hukumu.

²⁸ Na kama nikijisikia ya kwamba ninajua jambo fulani, na nisiwaambie, basi Mungu atanifanya niwajibike kwa ajili yake kwenye ile Siku ya Hukumu; na watu na mikono yao, wakisema, “Ndugu Branham, laiti ungalitwambia tu, tusingalikuwa katika hali hii leo.”

²⁹ Nataka kusimama kama Paulo wa kale, “Sina hatia kwa damu ya watu wote. Kwa kuwa sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.” Hiyo ni kweli, jinsi tu ninavyoliona; na iwapo nimekosea, basi Mungu anisamehe. Mambo haya kamwe hayaji... Kamwe sikwenda kwenye seminari yo yote ile, kamwe sikwenda kwenye shule yo yote, kamwe sikuchukua neno la mtu awaye yote juu ya jambo Hilo. Nilienda moja kwa moja katika Biblia, katika maombi. Basi jambo hili limefunuliwa Kiungu na Roho Mtakatifu, Malaika yule yule wa Mungu ambaye ananielekeza kuona maono na kadhalika namna hiyo, na kuponywa kwa wagonjwa. Nanyi

mnaweza kuamua kwa jambo hilo kama lingekuwa kweli ama si kweli.

³⁰ Naam, huu ni ujumbe wa yule malaika wa tatu, kwa ulimwengu. Nanyi mwajua nini, ujumbe wa malaika wa tatu, unaendelea sasa katika siku hizi. Huku ni kuruka kwa ujumbe wa yule malaika wa tatu, kama wewe ni msomaji wa Biblia.

³¹ Kulikuwa ole tatu zilizoufuata. Wa kwanza ulitukia kwenye Vita vya Kwanza vya Dunia. Wa pili ulitukia katika Vita vya Pili vya Dunia. Mnaona yale tunayoelekea sasa. Vema. Tumefikia mwisho wa njia.

³² Sasa hebu na tuliingize hili niani mwetu, kabla tu hatujasoma Maandiko. Mahali penyewe tulipo, hatuna budi kuwa katika wakati wa mwisho. Muda gani? Sijui; hakuna ajuaye.

³³ Lakini, angalieni, hebu kwa kuzungumzia tulichukue kihistoria. Miaka elfu mbili ya kwanza, taratibu ya ulimwengu ilifikia upeo wake, ndipo Mungu akauharibu ulimwengu kwa maji. Mnajua hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ndipo ukatokea kama ulimwengu mpya. Halafu miaka elfu mbili ya pili, ukafikia mwisho wake tena, ndipo Mungu akamtuma Yesu. Sivyo? [“Amina.”] Huu ndio mwisho wa miaka elfu mbili inayofuata, 1954. “Na Injili,” Yesu alisema, “kazi itafupishwa,” (kwa ajili gani?) “kwa ajili ya walioteuliwa, la sivyo hakuna mtu angeokolewa,” ungekuwa mbaya sana. Kwa hiyo tuko katika wakati wa mwisho. Kisha ule wa saba, katika mfano, ni ile Milki ya Miaka Elfu, miaka elfu.

³⁴ Kama vile Mungu alivyoshughulika miaka elfu sita, tunajua ya kwamba miaka elfu sita . . . “Siku moja Mbinguni ni miaka elfu moja duniani,” Petro wa Pili. Mnaona? Sasa, naye Mungu aliunenga ulimwengu katika miaka elfu sita. Nalo Kanisa lilishindana na dhambi sasa kwa miaka elfu sita. Na kwenye ile elfu ya saba, Mungu akaenda kupumzika, akapumzika katika ile elfu ya saba, na sasa mfano wa ile Milki ya Miaka Elfu, Kanisa kuishi hapa duniani, papa hapa katika umbo la mwili, kwa miaka elfu moja, bila maradhi, hofu, shida, wala mauti. Ule wakati mkuu wa ufanisi unaingia sasa! Loo, kwa ajili ya huo! Loo, ninaupenda ule wimbo:

Nchi inaugua, ikilia kwa ajili ya ile siku ya kuwekwa huru,
Wakati Yesu atakaporudi duniani tena.
(Napenda hilo.)
Dhambi na hofu, uchungu na mauti ya ulimwengu huu wenye giza vitakoma,
Katika utawala wenye utukufu pamoja na Yesu wa miaka elfu moja ya amani.

Biblia ilisema, “Walitawala na kumiliki pamoja na Kristo miaka elfu moja,” Milki ya Miaka Elfu.

Sasa, ujumbe huu wa malaika wa tatu, kabla tu ya kule Kuja kwa Bwana, wakati ile Muhuri na ile alama zilipotwiwa. Sasa, kutakuwa na kukusanywa kukuu, kukusanywa.

³⁵ Kule nje, kule nje Magharibi, wakati tunapoenda, nilizoea kwenda, nimeenda tangu nilipokuwa mvulana, kuenda kwa ajili ya kuwakusanya ng'ombe kwenye majira ya Kuchipuka majani na kwenye majira ya Mwishoni mwa mwaka, ninapanda milimani na kuwatelemsha ng'ombe. Na baada ya kuwapata ng'ombe wote tunaoweza kuwaona, kutoka kila mahali, ndipo tunawatenganisha nini hii wote. . . wale wasio wetu. Wetu wana alama, nao wametiwa alama. Na kama utawahi. . .

³⁶ Kuna mtu aliyepata kuwaona hao wakiwatia ng'ombe alama? Ni jambo la kushangaza sana kuwaangalia wakiwatia ng'ombe alama. Nilikuwa nikiwasikitikia hao ng'ombe. Na ni kazi kubwa na mchafuko wa kuchukiza sana unapoanza kuwatia ng'ombe alama. Kuchoma kile chuma cha kutilia alama ndiyo ilikuwa kazi yangu, kubeba kile chuma. Kisha kukibandika kwenye yule maksai mdogo aliyelala pale, huku miguu yake imefungwa; na kumtia alama hiyo, huku nywele na nyama zikiungua; tunatia lami kidogo juu yake, na kumwachilia. Basi nena juu ya kutimua mbio! Anatimua mbio kweli. Lakini, angalia, yeye ametiwa alama.

³⁷ Basi hivyo ndivyo Mungu anavyotufanyia sisi. Huna budi kushuka kwenda madhabahuni na kufungwa kama nguruwe, mara kwa mara. Lakini, ndugu, wakati Roho Mtakatifu anapokutia alama, huenda ukakimbia na kupiga makelele, bali umetiwa alama. Hiyo ni kweli. Uko pale. Bosi anapopita hapo, Yeye anajua wewe ni wa wapi.

Lakini, loo, kwa huyo mnyama anayetangatanga wa mwaka mmoja, huyo jamaa ambaye amehukumiwa kurudishwa kati ya wale wa—wa mashambani.

³⁸ Sasa, wakati wa kutia alama. Basi sasa kutakuwa na wapanda farasi wawili tu katika jambo hili, hao watakuwa Mungu na Shetani. Shetani atawachukua walio wake, naye Mungu atawachukua walio Wake. Usiku wa leo tutaona ni nani aliye na alama ya Shetani, na kesho usiku tutaona ni nani aliye na alama ya Mungu, kulingana na Neno la Mungu.

³⁹ Sasa huu hapa ujumbe wa yule malaika, aya ya 9 ya sura ya 14. Someni baadhi ya Maandiko haya hapa, niliyoyaandika. “Na malaika. . .”

Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au. . . mkono wake,

Yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; na. . . atateketeswa

kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo.

- 40 Hakika sitaki kuhusika na jambo hilo! Angalia.

Na moshi wa maumivu yao ulipanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila anayepokea chapa ya jina lake.

- 41 Sitaki kuhusika na jambo hilo hata kidogo, nina hakika. Naam. Sikilizeni aya inayofuata, huku nikiiangalia.

Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu Kristo.

- 42 Sasa sura ya 15, na aya ya 2. Kisha . . . Sikilizeni sasa, katika sura ya 15 na aya ya 2. Naam, tulikuwa tukisoma kutoka kwenye ya 14, na aya ya 9. Sasa ya 15, na aya ya 2.

Akaenda huyo wa kwanza, akakimimina kitasa chake juu ya nchi; pakawa . . . jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wanaoisujudia sanamu yake.

Sura ya 16 na aya ya 2.

Ambaye wafalme wa nchi wamezini naye, nao wakaa katika nchi wamelevywa kwa mvinyo ya uasherati wake.

- 43 Hebu kidogo. Samahani. Nilifungua, sina budi nilifungua mbili kwa wakati mmoja. Vema. Sasa sura ya 20 na aya ya 4. Vema, hii hapa.

Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao hao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu Kristo, na kwa ajili ya neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mkono yao; nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu.

- 44 Huwezi kupokea alama ya mnyama kisha umwabudu Kristo ama uwe pamoja Naye. “Bali mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama wala sanamu ya yule mnyama, atateswa mbele za Mungu na mbele za malaika watakatifu.” Hivyo ndivyo Bwana anavyosema juu ya jambo hilo.

- 45 Sasa tutaanza. Fungueni Biblia zenu sasa katika sura ya 13 ya Ufunuo, nasi tutaanza katika muda mfupi tu. Sasa jambo hili ni muhimu sana. Basi sikilizeni kwa makini sasa.

- 46 Kwanza, tunataka kuchukua somo letu kutoka usiku wa jana. Jana usiku tulichukua nyakati za kanisa, ambazo, jinsi tulivyomwona Yesu akisimama katika Kanisa Lake, “Akinena

kama sauti ya maji mengi; Naye alikuwa na nywele kama sufu; macho kama miali ya moto.”

47 Kumbukeni, yote yale—Ufunuo ni ono, na mfano. Yote ina maana, kwa hiyo huna budi kuangalia kwa makini. Soma manabii, uone kile ile mifano ilichoomaanisha, kisha ilinganishe upande huu ili kwamba ujue mifano hiyo inamaanisha nini hasa.

48 “Macho Yake yalikuwa kama miali ya moto,” yakienda huku na huko duniani. Nasi tuliona ya kwamba miali ile, kama... “Panga, upanga ulitoka kinywani Mwake, na upanga ukatao kuwili,” nasi tuliona kwamba huo ulikuwa ni Neno la Mungu lililotoka kutoka kwenye kinywa cha Kanisa. “Na hata lingekata mafuta yaliyomo kwenye mfupa, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo,” Waebrania sura ya 4.

49 Tulikuta Kanisa limesimama pale katika uzuri Wake; Kristo ameumbika tu ndani Yake! Nalo Kanisa lilikuwa limevikwa “nguo” nyeupe. Nanyi mnaona, Hilo lilikuwa ni mwanamke, “kifuani mwake,” lilikuwa na nguo iliyofunika aibu yake; na lilikuwa na “mshipi wa dhahabu,” hata hivyo, uliolifunga, uliolifunga matitini. “Nyeupe,” ikizungumzia juu ya haki ya Kristo; na “mshipi wa dhahabu” uliwakilisha Injili. Kuhubiri Injili kunamleta Roho Mtakatifu juu ya Kanisa, haki ya Kristo; unaishikilia hapo, limefungwa kwa kamba, mshipi wa kujifungia.

50 Halafu Yeye alikuwa amesimama juu ya, “miguu kama shaba, iliyokuwa imesafishwa katika tanuru.” Shaba inawakilisha hukumu ya Kiungu. Naye Mungu, ili kutuliza kile kiapo kikuu alichokula, Yeye alimtuma Kristo, ndipo Kristo akalipa ile hukumu ya Kiungu. Ndipo Kanisa lina msingi wake katika hukumu ya Kiungu, Kristo akisimama mahali Pake. Ni picha nzuri namna gani, “Akisimama katika Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu!”

51 Na basi tunaona ya kwamba, wakati wa kwanza wa kanisa, walichokuwa nacho. Ni wangapi waliokuwa hapa jana usiku, nione mkono wenu? Vema, hilo ni sawa. Wakati wa kwanza wa kanisa, tuliona, katika Wakati wa Kanisa la Efeso, wao walikuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nao waliwabatiza watu kwa maji, tena walikuwa na nini hii... Kila namna ya ishara na maajabu ilibidi ziambatane na mwamini.

52 Na jinsi, kwenye kila wakati wa kanisa, ilianza kufifia. Zamu ya pili, zamu ya tatu, kisha kupitia katika ule wakati wa giza. Ndipo wakatokea na jina la uongo, pamoja na ubatizo wa uongo, wa maji na wa Roho Mtakatifu pia.

53 Kisha wakashuka wakaja moja kwa moja, wakati uliofuata, nao wakaangaza kidogo. Kisha kukawa na mlango uliowekwa, upate kufunguliwa, kati ya Wakati wa Kanisa la Filadelfia na wa Laodikia.

54 Halafu la Laodikia likawa lenye uvuguvugu kisha likaenda nje moja kwa moja kutoka kote Mle, hata Mungu akalitapika kutoka katika kinywa Chake. Hiyo ni kweli. Hayo ni Maandiko.

55 Na kila mwanahistoria na kila mwamini halisi anajua ya kwamba Nyakati hizo Saba za Kanisa, ama “Vinara vya Taa Saba vya Dhahabu,” kama ilivyosema Biblia, vilikuwa ni zile Nyakati Saba za Kanisa. Kama vile Agano la Kale linavyoonyeshwa kwa mfano katika lile Jipya hapa, na vile lilivyokuwa linafifia.

56 Lakini kutakuwa na kutikiswa kukuu na ufufuo kabla tu ya kumalizika kwa majira ya Mataifa, kabla ya Wayahudi kuutambua tena.

57 Kumbukeni, Mataifa wako tu na wakati mfupi, wa neema. Biblia ilisema, “Wangekanyaga kuta za Yerusalemu,” Yesu alisema, “hata majira ya Mataifa yatakapokwisha.” Hiyo ni kweli. Kuna wakati uliopangwa wa kumalizia.

58 Nasi tunaona mambo waliyofanya kule nyuma. Tunaona ishara na maajabu zilizoambatana nao, jinsi Kristo alivyowaambia jinsi lilivyokukwa jambo la ajabu, na vile walivyokuwa. Kisha Nuru ikaangaza kufifia zaidi na zaidi, ikatoweka. Ndipo kwenye wakati tu wa kumalizia, ilikuwa kuwe na mlango mwingine uliowekwa wazi kwa ajili ya Kanisa. Sasa hebu tusimame papa hapa kabla hatujaingilia jambo hilo. Angalia, hebu tuchukue unabii mwingine ninaokumbuka. Nabii alisema, “Kutakuwako na siku ambayo itakuwa si usiku wala mchana.”

59 Ninapaza sauti sana? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Kama ukiweza, unaweza kuzima hiyo kidogo... Ninajua inarudisha mwangi, na hiyo ndiyo sababu ninazungumza kwa sauti kuu kidogo, ili kwamba watu walio upande wa nyuma wapate kulisikia. Kwa maana, Jambo hili ni muhimu sana.

60 “Na kutakuwako na wakati, siku,” nabii alisema, “ambayo haitakuwa usiku wala mchana.” Kwa maneno mengine, kungekuwa na nuru, bali itakuwa na mawingu, mnaona, siku yenye mawingu. “Lakini wakati wa jioni kutakuwako Nuru.” Ni picha nzuri namna gani!

61 Naam, wakati mchana ulipopambazuka kwenye siku hii yenye mawingu, hiyo inamaanisha kutakuwa na vita, na shida, na misukosuko, na majira, na makanisa, na itikadi, na kila kitu. Haitakuwa na nuru wala giza. Itakuwa ni wakati ambapo tunajua ya kwamba kuna Mungu, na kuna Injili, bali wao hawawezi tu kuyafahamu hayo. Mnajua ninalomaanisha? Wao watasema, “Biblia ilisema ya kwamba wao walifanya jambo *hilo* kule nyuma katika Pentekoste, walifanya *vile* katika kanisa la mwanzoni, wao walikuwa na ishara hizi na maajabu, lakini kanisa le—letu halifundishi jambo Hilo.” Mnaona, kuna mawingu, si usiku wala mchana. “Lakini, hata

hivyo, tunamwamini Yesu Kristo. Tunaamini katika Kuja Kwake mara ya Pili, nasi tunajua Yeye anakuja.”

⁶² Biblia ilisema, “Haitakuwa mchana wala usiku.” Usingeweza kuiita mchana, wala usingeweza kuiita usiku. Lakini, angalia, “Wakati wa jioni kutakuwako Nuru,” wakati wa jioni!

⁶³ Wakati watu wa mashariki... Kitabu hiki ni Kitabu cha mashariki; ndivyo ilivyo Biblia. Wakati Nuru ilipojitokeza katika Kanisa la mwanzoni, katika Efeso, vema, tunakumbuka na tumeona kile kilichotukia pale; Nuru ya Mungu iliyoletwa kwa njia ya Yesu Kristo, kwa kule kumwagwa kwa mara ya kwanza kwa Roho Mtakatifu. Kulitoa Nuru kwa ulimwengu wote, na kuandika Biblia. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.]

⁶⁴ Sasa Yeye aliahidi, katika ulimwengu wa magharibi, jua huchomoza mashariki, mwanzoni mwa majira ya neema, na sasa jua linatua magharibi, kwenye watu wa magharibi. Sisi ni watu wa magharibi. [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara tatu—Mh.] Naye aliahidi ya kwamba kutakuwako na ufufuo na kungekuwako Nuru wakati wa jioni. Ziko hapa. Nuru inaangaza, “wala giza haliwezi.” Ndivyo hivyo. “Watu wanapenda matendo mabaya zaidi kuliko wanavyoyapenda matendo mazuri.”

⁶⁵ Lakini iko karibu kutua kwenye upeo wa macho kule ng’ambo. Nayo Nuru ndogo tuliyo nayo, ishikilieni Hiyo. Angalieni, ni jua lile lile lililozuka kule ng’ambo kwa Wayahudi, linalotua hapa kwa Mataifa. Katika wakati wote hapa, kupitia miaka hii elfu mbili, wao walikuwa na *hili*, na *lile*, na madhehebu na majira, na *hili* na *lile*. Na watu hawajui wanakosimama.

⁶⁶ Lakini Biblia inaahidi, Mungu aliahidi, kupitia kwa nabii, ya kwamba, “Wakati wa jioni kutakuwako Nuru.” Kutakuwako Nuru wakati wa jioni. Ninaamini tumefika. Jua linatua. Maumbile yote yanaugua, yakililia ile siku. Angalieni.

⁶⁷ Sasa tunaona, ya kwamba, walichokuwa nacho huko kwenye ule wakati wa kwanza kabisa wa kanisa, walikuwa na fundisho geni. Muda si muda, likawa tu “matendo” fulani. Yeye alisema, “Unayachukia matendo ya Nikolai.”

⁶⁸ Sijui Wanikolai walikuwa nini? Nilitafuta hilo, na katika historia, kila mahali, nikasoma maelezo mazuri sana niliyoweza kupata, wala hakuna awezaye kujua, isipokuwa liwe ni fundisho lililoanzishwa na mtu fulani, Nic, Nicolas, ambaye alidhaniwa kuwa mmoja wa mitume ambaye kwa namna fulani alipotea. Yeye alianzisha kanuni ya imani, ama kitu kama hicho, na kutoka hapo wakatokea Wanikolai. Ilikuwa ni matendo, kwanza. Na yaliyokuwa “matendo” katika Waefeso, katika wakati uliofuata wa kanisa yakawa “fundisho.” Kisha yakaingia kwenye wakati wa giza wa mateso.

⁶⁹ Sasa fundisho lilo hilo la Nikolai lililoanza hapa katika kanisa la kwanza, baada ya zamu za kwanza tatu nne za mitume, likawa tendo. Wakaanza kuwazia, “Vema, *hili* Ndilo.” Sasa ninyi nyote mnajua jinsi jambo hilo lilivyotukia, nanyi wasomaji wa Biblia.

⁷⁰ Naam, ilianzia yapata A.D. 600 na . . . ama 306, wanachokiita kuongoka kwa Constantine. Yeye hakuongoka kamwe. Jamaa ambaye angefanya mambo machafu ambayo mtu huyo alifanya, hakuwa ameongoka. Hiyo ni kweli. Jambo tu alilowahi kufanya, lililokuwa na udini wo—wo wote, aliweka msalaba kwenye kanisa la Mtakatifu Sofia. Hivi hilo halikuwa jambo kweli, la kumfanya aende Mbinguni? Vema. Yeye aliwaambia Wakristo, endapo atashinda vita hivyo, atakuwa Mkristo. Nao wakaomba. Akatoka akaenda akashinda vita, ama akashinda yale mapigano, kisha akarudi akasema, “Vema, nitajiunga na kanisa.” Ni mfano mzuri sana wa mfuasi wa kanisa mwenye uvuguvugu leo. Hiyo ni kweli. Akaweka msalaba juu ya kanisa.

⁷¹ Baada ya kifo chake . . . Yeye alikuwa na wana wawili, wana watatu; Constantine, Constatius, na Constans-tinople, ambao walianzisha kuunda magharibi na mashariki ya Rumi, nao wakatengana. Ndipo mle ndani, basi, kukatokea Dola ya Ottomani, mnamo wakati huo.

⁷² Halafu basi, wao, yapata zamu ya pili, ama ya tatu, zamu ya nne ya mitume; halafu, muda si muda, wakaaza kuzozana wao kwa wao. Ndipo wakatengana, itikadi ndogo.

⁷³ Kila mtu, chukua kanisa . . . Hapo, wakati kanisa hilo la Methodisti ya Kiwesley lilipokuwa linatawala, lilikuwa linatawala wakati John Wesley alipokuwa hapa. Waluteri walikuwa wanatawala, katika siku yao; na kila mmoja. Lakini acha mwanzilishi afe, wakati mmoja, ndipo wanapotea.

⁷⁴ Wakati Bwana alipotokea kule nyuma; walipotaka mimi nianze, niunde madhehebu juu ya jambo Hili, na kadhalika namna hii. Nilipanda kwenda kule, nikaona mahali ambapo Dwight Moody, mwazilishi mashuhuri, Chuo Cha Biblia Cha Moody. Ndipo nikawaza, “Kama Dwight Moody angeweza kuangalia Chuo hiki cha Biblia; kile mtu huyo alichotetea, na yale wanayofanya siku hizi!”

⁷⁵ Vema, nilisema, “Angalia hapa, angalia, vipi kama—vipi kama Wesley, Calvin, Knox, Finney, Sankey, ama Finney, ye yote wao, angalifufuka leo, na kuona mahali kanisa lilipo!” Loo, jamani! Mnaona, zamu ya kwanza, wakati huyo mtu anasimama pale, yeye anashikilia ile Kweli.

⁷⁶ Mwangalie Dr. Dowie katika Mji wa Zayuni, mbona, kicheko dhahiri katika kuponya Kiungu, wakati ule m—mji ulikuwa umewekewa msingi juu ya jambo hilo. Lakini Dowie alipokufa, ndipo kukazuka kile . . . Blake, John Lake na hao wengine wote. Basi muda si muda, limejizungusha kila mahali sasa hata

Assemblies of God limeingia mle, na kundi kubwa la watu baridi na kila kitu. Nalo ka—kanisa limekwisha na kurudi nyuma, nalo liko katika hali ya kuchukiza.

⁷⁷ Kwa hiyo nikaona jambo hili, Biblia ilisema, “Daudi alimtumikia Bwana vizuri katika kizazi chake.”

⁷⁸ Kwa hiyo nikasema, “Bwana, sitaki madhehebu yo yote. Nijalie nikutumikie Wewe kwa moyo wangu wote, wakati niko hapa ningali hai.” Hiyo ni kweli. “Jambo la pili, Wewe utampata mtu mwingine nitakapoondoka. Utampata mtu mwingine kuchukua mahali pake.” Hivyo tu.

⁷⁹ Usijaribu kujenga juu ya mwingine. Huwezi kuwasha moto mahali pale pale. Iliwabidi Israeli kuendelea kusonga mbele. Wakati waliposimama, wao wakarudi nyuma. Iliwabidi kuendelea kusonga mbele kila usiku; wakawasha moto mpya kila usiku; wakaendelea tu kusonga mbele. Basi hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya. Kile alichokuwa nacho Luther kilikuwa sawa; hicho kilikuwa ni kwa ajili ya siku ya Luther. Kile alichokuwa nacho Wesley kilikuwa sawa; hicho kilikuwa ni kwa ajili ya siku za Wesley. Walichokuwa nacho watu wa utakatifu, hicho kilikuwa sawa; hiyo ilikuwa ni siku yao. Tunaishi katika siku nyingine. Sasa tuna—tunasonga mbele. Na ikiwa kuna siku baada yetu, itakuja vile vile. Lakini hebu tutembeo Nuruni wakati Nuru iko hapa sasa.

⁸⁰ Nami ninaona hivi, ya kwamba, mle ndani fundisho hili likazaliwa, muda si muda, mpaka likaingia katika furushi la itikadi, ndipo Warumi wakaongoka. Naam, dola ya Kirumi, tangu siku zile za—za Rumi kuutwaa na kuushinda ulimwengu wa Mataifa kutoka kwa Uyunani, baada ya kuanguka kwa Alexander Mkuu, limekuwa taifa linalotawala ulimwengu; Warumi, wakati wa Mataifa. Danieli alinena hayo, katika ono. Tatalifikia, katika—katika dakika chache. Lakini daima limekuwa linaloutawala ulimwengu; Warumi.

⁸¹ Ndipo tunaona pale, basi, ya kwamba walilifanya kanisa madhehebu. Kundi la watu lilikutanika, yapata 606, na kujiita wenyewe, “mapadri wa mwanzoni,” mapadri wa kanisa. Kundi la watu lilikutanika na kufanya baraza juu ya yale wanayopaswa kufanya, nao wakaunda madhehebu.

⁸² Basi hebu nizungumze hapa, rafiki zangu Wakristo, Waprotestanti na Wakatoliki pia. Na sasa, nafikiri nina marafiki Wakatoliki wanaoketi hapa; sisemi jambo hili kuwaudhi. Maana, tulieni tu kwa dakika chache, nasi tutayapata Maskani ya Branham mle ndani pia, mnaona, kwa ngojeni kidogo tu. Tunapaswa tu kuihubiri Injili jinsi ilivyowekwa hapa. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tano—Mh.] Haidhuru ni wapi. . . Yohana alisema, “Shoka lilikuwa limewekwa kwenye shina la mti,” wacha vipande viruke vitakako. Hiyo ni kweli. Yeye hana budi kuikata miti na kadhalika.

⁸³ Lakini, angalieni, mle ndani wao walilifanya kanisa la kwanza madhehebu. Nao wakakusanyika wakalifanya madhehebu kanisa la kwanza, ambalo liliitwa kanisa la dunia nzima, ama kanisa Katoliki huko Rumi. Nalo Katoliki linasema ya kwamba ni “kanisa mama.” Na hiyo ni kweli kabisa. Ndilo kanisa mama la madhehebu. Kweli. Ndio mara ya kwanza, katika historia yote ya ulimwengu, ambapo palikuwa na kanisa lililofanywa madhehebu; hakukuweco, tangu mwanzo wa wakati.

⁸⁴ Katika siku za Israeli, wao hawakuwa ma—hawakuwa madhehebu. Walikuwa jamii, si madhehebu. Nao. . . Yesu Kristo kamwe hakufanya kanisa madhehebu. Hakuna mmoja wa wale mitume aliyepata kufanya kanisa madhehebu. Na hakuna wakati wo wote, baada ya vizazi vitatu vinne vilivyowafuata, walipofanya kanisa madhehebu. Nakutaka ulete historia na uelekeze kidole kwenye. . . Nionyeshe mahali lilipo. Nami nimesoma Josephus na wanahistoria wote mashuhuri tulio nao ulimwenguni leo, niwajuao, maana sina budi kuwa na hakika. Ninatoa tamshi hili mbele ya maelfu ya watu; huna budi kuweza kuunga mkono na kuthibitisha kile unachonena. Hiyo ni kweli. Hakukuweco na madhehebu kamwe. Wala hamna. . .

⁸⁵ Pia Mtakatifu Petro hakuanzisha kanisa Katoliki kamwe. Ninataka historia moja, ama Andiko hata moja. Mtakatifu Petro alikuwa mtu aliyeoa. Mlisema yeye alikuwa papa. Asingeweza kuwa papa. Petro alikuwa mtu aliyeoa. Biblia ilisema mama ya mkewe alikuwa anaugua ho—homa, ndipo Yesu akamponya.” Na kadiri ni juavyo mimi, Mtakatifu Petro hakuwahi kufika Rumi kamwe. Wala hakuna historia inayoonyesha kamwe kwamba alikuwa Rumi. Basi hilo ni kosa.

⁸⁶ Lakini wao waliunda madhehebu na kuweka kanisa linaloitwa kanisa la dunia nzima. Hapo wao walifanya sala ya watu wote. Walikuwa na upatano mkamilifu; kila mtu alipaswa kuwa katika umoja, kila mtu aseme jambo lile lile. Sala ile ile ilisemwa.

⁸⁷ Nao wakatengeneza kundi la Maandiko, wakiyachukua kutoka katika Biblia, mengi ya hayo, na kutunga mengine. Hakuna pargatorio iliyotajwa hata mara moja katika Vitabu vyote vitakatifu vya Biblia; hakuna “salamu Maria,” hakuna kitu kama hicho. Daima ni kinyume, dhidi yake, kila mahali katika Maandiko. Hapajakuweco, wakati wo wote. Na endapo utapata mahali pamoja, una haki ya kuja kesho usiku ukanisahihishe. Hakuna, mahali po pote; mlete kasisi wako ama mchungaji. Hakuna mahali, katika Maandiko, ambapo jambo hilo limewahi kutajwa.

⁸⁸ Kitabu kidogo tu, cha Makabe, kilichoongezwa kwenye Hii, ambacho hakijavuviwa; mambo yaliyoongeswa kwenye Hii, ama kuondolewa kutoka katika Hii. Biblia *Hii* ndiyo ya Peeke. Ile. . .

Imetambuliwa na wale waanzilishi wa mwanzoni, ama ye yote wa wanahistoria wa kanisa la mwanzoni, ama wakati wote wa Wayahudi wa Kiorthodoksi, nao hawakutambua cho chote ila Biblia hii tuliyo nayo leo.

⁸⁹ Sasa, basi, katika jambo hilo, sikilizeni kwa makini sasa. Sasa mnafikiri Katoliki inacharazwa? Hebu kidogo, mnaona.

⁹⁰ Sasa, ndipo wakalifanya kanisa Katoliki madhehebu, halafu wakaanza mateso, ambayo wao... Ilikubidi kumfanya kila mmoja, kila mahali, kanisa na taifa, viungane pamoja, na kuingizwa kutoka Rumi ya kikafiri kuingia katika Rumi ya kipapa. Kwa maneno mengine, kutoka kwenye ushirikina wa kipagani, wao waliuchukua Ukristo katika mtindo wao wenyewe. Mnaona? Wasingeelewa kwa nini mtu huyo angesimama na kutoomba kwa kitu cho chote. Walikuwa wapagani, kwa hiyo waliondoa tu Venus wakaweka Mariamu; waliondoa Jupiter, wakamwinua Petro; namna fulani ya sanamu ya kusujudia. Naam, nao wakasujudu mbele ya kitu hicho. Ndipo waka tengeneza sala ya watu wote, wakaisema katika Kilatini isije ikashindwa, na kadhalika. Wao daima wanaisema ile ile.

⁹¹ Nawe huwezi kuzungumza wala kuhojiana na kasisi wa Kikatoliki, wala Mkatoliki ye yote yule, juu ya msingi wa Biblia.

⁹² Mmoja aliketi, kijana huyu kasisi hapa, aliketi nyumbani mwangu hivi majuzi tu. Akasema, "Ninyi Waprotestanti, mnasoma Biblia kisha mnakaa nyumbani. Sisi Wakatoliki tunaenda kanisani na kuabudu."

Nikasema, "Lakini ni nini? Hivyo ndivyo ilivyo. Sasa nijibu hilo."

Akasema, "Mungu yumo katika kanisa Lake."

⁹³ Nikasema, "Yeye... Hakuna hata chembe moja ya Maandiko inayosema jambo hilo." Nikasema, "Mungu yumo ndani ya Neno Lake. Yeye alisema, 'Kila neno la mwanadamu liwe uongo, nalo Langu kweli.'"

⁹⁴ Akasema, "Hivi hufikiri kundi zima la watu, wakishauriana kwa pamoja, wangekuwa na mamlaka zaidi ya mtu mmoja?"

⁹⁵ Nikasema, "La. Kama mtu huyo mmoja yuko katika mapenzi ya Mungu, yeye yuna ile Kweli." Daima hilo lilithibitishwa.

⁹⁶ Kama vile Yehoshafati na Mikaya, yale masomo ndiyo kwanza tuwe nalo juzijuzi, Jumapili iliyopita, wakati Mikaya alipopanda akaenda kule. Huku wahubiri mia nne wakisimama, wakisema, "Kwea! Bwana yu pamoja nawe. Kwea! Bwana yu pamoja nawe."

Yehoshafati akasema, "Hivi hakuna mmoja zaidi hapa?"

Akasema, "Yupo Mikaya, lakini namchukia."

Kasema, "Hebu tusikie analosema."

Kasema, “Kweeni, lakini niliwaona Israeli wametawanyika kama kondoo.”

Kasema, “Hivi sikukwambia?” Unaona?

⁹⁷ Kwa hiyo, ni nani aliyekuwa sahihi, pale? Wakati manabii mia nne waliofunzwa wamesimama pale mbele ya huyo mtu, hata hivyo maskini mtakatifu mmoja anayejifingirisha na mkali aliyesimama kule nyuma alikuwa na ile kweli. Hiyo nikweli. Hiyo ni kweli. Alikuwa nayo. Alikuwa na ile kweli. Alipigwa kofi la mdomoni na kupigwa, juu ya jambo hilo, bali yeye alikuwa na ile kweli.

⁹⁸ Kwa hiyo haijalishi ni wangapi wanasema *hili*, ama ni wangapi wanasema *lile*, ni kile BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Itakubidi kusimama peke yako, mara nyingi, unaposimama juu ya Neno la Mungu, lakini hakikisha umesimama juu ya yale Bwana amesema.

⁹⁹ Naam, wao walilifanya kanisa hili madhehebu, kundi kubwa, kanisa Katoliki, ambalo linatawala dini zote, leo, katika milki ya Kikristo, ni Ukatoliki. Lakini wao wanasema, “Huhitaji... Sisi hatunini hii...”

¹⁰⁰ Unasema, “Mnapata wapi ‘kutokula nyama’? Mnapata wapi ‘kasisi kutokuoa’? Mnapata wapi jambo hili?”

¹⁰¹ Kasema, “Sisi hatufundishi Biblia.” [Ndugu Branham anagonga mimbara mara kadha—Mh.] Kasema, “Kanisa ndilo sauti. Haidhuru Biblia inasema nini; ni yale kanisa lisemayo.”

¹⁰² Bali Mungu alisema, “Na kila neno la mtu liwe uongo, na Langu kweli.” [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tatu—Mh.] Sasa huna budi kujichagulia.

¹⁰³ Naam, Nikolai hiyo ilikuwa imekuwa fundisho, kisha ikawa mateso, Sasa, hii hapa inajitokeza katika siku za mwisho. Ndipo kukatokea faraja, kupitia kwenye nyakati za giza na mateso; kisha kukaja kuachilia, kwenye yale matengenezo ya kwanza, ambayo yalikuwa ni Martin Luther. Martin Luther alilipinga kanisa Katoliki, kwa sababu hiyo alienda kule na kuchukua ule ushirika...

Nao wakasema, “Huu ni mwili wa Kristo.”

¹⁰⁴ Akasema, “Si mwili wa Kristo. Ni mkate mwembamba, na hivyo tu ndivyo ulivyo.”

¹⁰⁵ Wao wanaamini ya kwamba ni ukaristi takatifu, ambayo, “*Ukaristi takatifu* maana yake ni ‘Roho Mtakatifu.’ Na unapopokea hiyo, unamchukua Roho Mtakatifu mwilini mwako.” Na hilo ni kosa.

Roho Mtakatifu ni ubatizo wa Roho.

¹⁰⁶ Si, “Hata ilipotimia Siku ya Pentekoste, kasisi akapanda akaja akawapa ukaristi takatifu, mkate mwembamba kwenye

ulimi wao.” Wala si, “Mhubiri fulani akaenda akawanyunyizia maji kidogo, akawapa mkono.” La, bwana.

¹⁰⁷ “Lakini kukaja toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ulioijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.” Hayo ni Maandiko. Hayo ndiyo yaliyo kweli. Hivyo ndivyo ilivyotukia katika Kanisa hilo, na hivyo ndivyo imetukia wakati ile Nuru inaangaza katika siku hii. Hapo ndipo ile Nuru ilipochomoza; na hapa ndipo ile Nuru inapopenyeza kupitia hapa.

¹⁰⁸ Sasa kama Maandiko yo yote, ninayonukuu, yakitiliwa swali, yawekeni tu kwenye...Nitawapa mahali yanapopatikana, mnaona, katika Maandiko. Vema. Bila shaka, katika tu wakati mdogo kama huu...Kwa kawaida, tutakapomaliza kuuchambua Huo, tunachukua majuma kadha na miezi kadha. Kila Andiko tu, tunalifuatilia, watu wakiwa na Biblia yao. Lakini, kama likitiliwaswali, hebu tu nijue. Vema.

¹⁰⁹ Ndipo, Martin Luther. Ndipo, baada ya Martin Luther, akaja Wesley.

¹¹⁰ Martin Luther alitokea na katekismo, mambo chungu nzima. Alitoka na ubatizo, alitoka akifundisha utatu, ubatizo wa utatu ambao kamwe haukufundishwa katika Biblia, kamwe haukufundisha katika Biblia. Hakuwapata kuwa na mtu ye yote aliyepata kubatizwa katika ubatizo wa miungu watatu, katika Biblia. Kama ndivyo ilivyo, njoo unionyeshe ni wapi. Halipo.

¹¹¹ Jinsi tu walivyoagizwa kubatizwa, ilikuwa ni, “Enendeni mkawafanye mataifa yote wanafunzi,” alisema kule nyuma, “mkawabatize katika Jina,” si jina, “katika Jina; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Nao wanafunzi wakageuka moja kwa moja wakambatiza kila mtu katika Jina la “Yesu Kristo,” na wakaagiza ya kwamba kama mtu ye yote alikuwa amebatizwa kwa njia nyingine yo yote, ilimbidi kuja na kubatizwa tena kabla hawajaweza kumpokea Roho Mtakatifu. Ndipo hili hapa kanisa Katoliki linatoka... .

¹¹² Weka mahali pamoja katika Biblia ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa katika Jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Hilo ni wazi sana, sivyo? Jumamosi usiku ni usiku wa maswali, nitalipata, tutalinyosha hilo. Sawa. Sawa. Nataka mtu ye yote anayeweza kunionyesha mahali pamoja ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” nitaondoka mimbarani niseme mimi ni mnaofiki. Mtu ye yote aliyepata kubatizwa kwa njia nyingine yo yote, ilimbidi kuja na kubatizwa tena katika Jina la “Yesu Kristo,” kumpokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli kabisa. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema.

¹¹³ Naam, mnaona, tunachukua nadharia badala ya Kweli. Sasa angalieni katika Maandiko. Msiseme, ati, “Vema, Ndugu

Branham alisema.” Angalieni Maandiko sasa. Chukueni kamusi yenu mkachunguze jambo hilo. Halafu basi mara . . .

¹¹⁴ Angalia, kila mmoja wa hizo nyakati za kanisa ulikuwa na Jina Lake, mpaka likapitia katika wakati huu wa giza wa kanisa.

¹¹⁵ Basi, angalia, huko kuonyesha katika mfano katika—katika kanisa la Kiothodoksi. Hapo ule wakati wenye giza kuliko zote ulipokuwa unaendelea, wa Wayahudi, ilikuwa ni wakati Ahabu, baada ya ile fanaka baada—baada ya yule mfalme mkuu aliyemtangulia; na kabla ya wakati huo, Israeli ilikuwa katika hali ya kupendeza kabisa. Ndipo Ahabu akaingia kama mwamini wa mpakani, hali ya uvuguvugu, kisha akapanda akaenda na kumwoa maskini binti mfalme huyu, Yezebeli, ambaye alikuwa mwabudu sanamu, akamwingiza, ndipo akaingiza ibada ya sanamu katika Israeli. Hivi hamkumbuki jambo hilo? Mfano mzuri sana.

¹¹⁶ Hapo Uprotestanti ulipoolewa na Ukatoliki, wao walileta ibada za sanamu tena katika Ukristo, katika ule wakati wa giza; sawa kabi—kabisa, kijeografia.

¹¹⁷ Sasa angalia wakati linapotokea upande huu. Hapa una nini? Badilisho la Roho Mtakatifu; mkate mwembamba. Badilisho la ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Wao walibadilisha kila kitu. Ninaweza kuchukua na kuthibitisha kwa Maandiko; badilisho baada ya badilisho.

¹¹⁸ Naye Martin Luther alikubaliana na jambo hilo. John Wesley alikuja moja kwa moja na jambo lile lile, akakubaliana nalo. Kamwe hakujakuwa na mtu ye yote, katika Biblia, aliyewahi kunyunyiziwa. Hapajatokea jambo kama hilo kamwe. Hapakuwepo na kitu kama hicho kwenye Biblia, hakuna agizo wala amri ya jambo hilo kabisa, bali ninyi mnaliruhusu. Hiyo ni kweli. Mnaliruhusu. Wao wanatoka wanakuja wanachukua chombo hiki cha maji ya chumvi na kuwanyunyizia. Kwa nini? Kanisa Katoliki lilianzisha jambo hilo, nanyi mnalikubalia. Kweli.

¹¹⁹ Jamaa mmoja alisema, hivi majuzi, kasema, “Wewe si . . . Wewe, wewe si Mkatoliki. Wewe ni . . .”

¹²⁰ Nikasema, “La, ndugu. Mimi ni Mprotestanti. Ninapinga kitu hicho.” Hiyo ni kweli. Kama mhudumu wa Injili, nikiwa na watoto wa Mungu kama wanafunzi wangu hapa, wanaoelekea Mbinguni, nami inanibidi kuwahubiria na kuketi mbele yao kama mwalimu nikiwa na ishara na maajabu, ningekuwa mnafiki kama sikutetea yaliyokuwa kweli. Nikasema, “Naam, bwana. Nitasimama, hata jambo hilo liniuwe. Nitasimama. Nita—nitafundisha tu yaliyo ya Biblia.”

¹²¹ Nami niko tayari, wakati wo wote, kulizungumza jambo Hilo na mtu ye yote, mnaona; hata iwe ni papa wa Rumi, ama askofu mkuu, ama ye yote yule. Mnaona? Naam, bwana. Hiyo ni kweli.

Endapo nimekosea, njoo unionyeshe. Naam, sijakosea, maana ninayanukuu Maandiko. Wewe... Sitachukua kitabu chako cha mafundisho. Hiki ndicho Kitabu cha mafundisho, papa hapa. [Ndugu Branham anagonga-gonga mara nne—Mh.]

¹²² Naam, basi, unaona, wao walianza kutoka wakiwa na mambo haya yote ya kawaida.

Naam, katika siku za mwisho, kutatokea mateso.

¹²³ Sasa tuko, karibu, Ufunuo sura ya 13 sasa, kwanza. Sasa kama utaangalia, kuendelea kwenye sura hii hapa, kasema, “Nikaangalia, na tazama, Mwana-Kondoo alisimama juu ya mlima Sinai...” La, samahani, niko kwenye aya nyingine, sura nyingine, ya 14. Sura ya 13:

...nikasimama juu ya mchanga wa bahari, *nikaona mnyama* anatoka katika bahari, *mwenye pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi, na juu—juu ya vichwa vyake majina ya makufuru.*

¹²⁴ *Makufuru* ni nini? Ni “kucheka, kudhihaki, kunena juu yake.” Sasa angalia, alikuwa na “vichwa saba, pembe kumi.” Halafu angalia wakati anapotoka “katika bahari.” Sasa Ufunuo 17, ninyi ambao mnaandika jambo hilo, 17:15, kasema ya kwamba yale—ya kwamba yale *maji* yanawakilisha “umati na makutano ya jamaa.” Kwa hiyo *mnyama* huyu anawakilisha “nguvu, nguvu zisizo za Kiungu.” “Mnyama mkali aliinuka miongoni mwa watu, kisha akasimama kwenye mchanga wa bahari. Nami nikamwona mnyama...”

Na yule mnyama niliyemwona alikuwa mfano... chui, ... miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu, ... kinywa chake... kinywa cha simba; yule joka akampa nguvu zake na kiti... cha enzi na uwezo mwingi.

¹²⁵ “Yule joka!” Tuna mambo mawili tunayoyachunguza sasa. Mwangalie mnyama huyu. Alikuwa na tabia nne mbalimbali ndani yake.

¹²⁶ Basi mkichukua Danieli 7, ninyi ambao mnaliandika, Danieli 7. Danieli aliona ono lile lile, miaka mia nane kabla ya jambo hili, aliona hilo ono. Aliwaona wanyama hao, wakiwa mbalimbali, mmoja kwa mwingine, mwanzoni mwa utawala wa Mataifa.

¹²⁷ Nao hawa hapa, Yohana akiliona, na mwisho wa... [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]... wa utawala wa Mataifa, wanyama hao wote wanne wakiwakilishwa katika mmoja. Pepo wale wale wa kale, pepo walioupagaa kila ufalme wa Warumi, toka zamani, na Wayunani, na kadhalika, na toka zamani katika majira ya Mataifa, wamekuja moja kwa moja na wote wakakutana katika mnyama mmoja. Tutampata, moja kwa moja, na tuone ni nani. Sawa. Wote hao, chui, simba, wote hao ni yule joka. Ni wangapi wanaojua joka ni nini? *Joka* linawakilisha “Rumi.” Naam.

128 Hebu—hebu na tusome jambo hilo. Hilo, hilo kwa namna fulani linatiliwa swali moyoni mwenu. Nipeni Ufunuo sura ya 12, kwa muda mchache tu hapa. Hebu tuangalie hapa, Ufunuo 12. Sasa angalieni.

Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke. . .

129 *Mwanamke* anawakilisha nini? “Kanisa.” Huyu ni—huyu ni bibi-arusi hapa. Hili ni kanisa, kanisa halisi.

. . . mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, . . .

130 Angalia, mwezi chini ya . . . “Jua kwenye kichwa chake, mwezi chini ya miguu yake.” *Jua* lilikuwa yale “majira ya neema.” Nao *mwezi* ulikuwa yale “majira ya torati.” *Mwanamke* alikuwa ni “kanisa la Kiothodoksi,” naye alikuwa amesimama juu ya torati. Torati ilikuwa inapita, maana torati ilikuwa ni kivuli cha mambo mazuri yajayo. Sivyo? Mwezi ni kivuli tu, cha jua likirudisha mng’ao kwenye mwezi (sivyo?), likiufanya mwezi. Nayo torati ilikuwa chini ya miguu yake; alikuwa ameisha pitia maisha ya siku hiyo. Basi angalia jinsi alivyokuwa amealia hapa sasa.

. . . na chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili. (Kanisa limevikwa taji kwa Fundisho la wale mitume kumi na wawili, mnaona.)

Naye alikuwa na mimba, akilia, hali ana utungu na kuumwa katika kuzaa. (Hilo lilikuwa kanisa la Kiorthodoksi. Angalia.)

I—ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu, alikuwa na vichwa saba. . . (mnaona, wekeni hiyo saba mawazoni mwenu sasa, “vichwa saba,” kila mara). . . *vichwa saba. . . pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba.*

Naam, na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi. Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake. (Angalia!)

Naye akazaa mtoto mwanamume, yeye atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Na mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi.

131 Kanisa la Kiothodoksi likisimama pale; jua likiangaza chini; Fundisho la wale mitume kumi na wawili. Sawa. Huku mwezi ukiwa chini ya miguu yake, torati, kivuli cha mambo yajayo; Nuru ya Injili ikiangaza sasa, torati ilififia wakati *Jua* lilipochomoza.

132 “Alikuwa na utungu wa kuzaa, kisha akamzaa Mtoto Mwanamume,” ambaye alikuwa ni Kristo Yesu, “naye akanyakuliwa hata kwa Mungu. Lakini mara. . .” Hili hapa.

“Mara yule joka, ambaye alikuwa ni Ibilisi, alipomwona yule mwanamke yuko tayari kuzaa, alisimama moja kwa moja karibu naye apate kumla Mtoto Wake mara alipozaliwa.”

¹³³ Na wakati Yesu alipozaliwa, Dola ya Kirumi ilitoa tangazo, kuwauwa watoto wote tangu umri wa miaka miwili, kwenda chini, ipate kumuua Kristo Yesu. Ndipo Mungu akamhadaa, akamchukua akampeleka huko Misri akamficha, kama Yeye alivyomfanya Musa vile vile.

¹³⁴ Hilo hapo lile joka jekundu, Ibilisi. Kiti chake kiko wapi, huko? Si Urusi; huko Rumi! Kisha kasema, “Ibilisi akampa kiti chake na mamlaka yake, joka jekundu,” si Urusi.

¹³⁵ Ninawasikia wahudumu mashuhuri wakisema, “Urusi ndiyo mpinga Kristo.”

¹³⁶ Mbona, Urusi haina uhusiano wo wote na mpinga Kristo. Huo ni ukomunisti. Uongo wa Uprotestanti na Ukatoliki ndio umesababisha ukomunisti. Sababu ya Urusi kuwafukuza kutoka kule, ni kwa kuwa wao walikuwa na pesa zote. Na sala zote zilifanywa katika watakatifu hao, hivi kwamba walijenga mijengo iliyo mikubwa sana, nao walikuwa na utajiri wote wa watu, na kuulundika namna hiyo. Nao wakaona kwamba hawaishi tafauti, wala hawakuwa tofauti na walimwengu wengine, nao wakawatapika na kuunda ukomunisti.

¹³⁷ Sasa kama mtanipa usiku mwingine mmoja, kama Mungu akinipa, nitawathibitishia ya kwamba ukomunisti unatenda kazi moja kwa moja katika mikono ya Mwenyezi Mungu, kuuangamiza Urumi. . . Pia, kumbukeni, ninasema jambo hili kama nabii wa Mungu, dola ya Urusi itaangusha bomu la atomiki ya namna fulani juu ya Mji wa Vatican na kuuangamiza katika saa moja. BWANA ASEMA HIVI. Nayo Biblia ilisema ya kwamba Mungu aliwachukua hao watu wenye mioyo ya kikatili na kuwaweka mikononi Mwake, nao walikuwa vyombo mikononi Mwake, “kutimiza mapenzi Yake,” na kumrudishia kile hasa kilichokuwa kinamjia. Hiyo ni kweli kabisa. Hilo ni Neno.

¹³⁸ Ndugu, hutambui tu jinsi mambo haya yalivyo na hila! Kumbuka, Yesu Kristo alisema ya kwamba Mpinga Kristo angefanana sana hata jambo hilo lingewapoteza walio wateule. Kasema, “Basi msiache mtu ye yote awashawishi.” Kasema, “Msiwe kama watu wa mataifa, kupayuka-payuka katika maombi yenu, ‘Salamu Maria, umebarikiwa, umejaa neema, na amebarikiwa. . .’” Kasema, “Msiwe kama watu wa mataifa, mkipayuka-payuka bure.” Akasema, “Wala msimwite mtu ye yote ‘baba,’ wa dunia hii, pia, wala. . .kwa kuwa mna Baba mmoja, aliye Mbinguni.”

¹³⁹ Lakini mnageuka na kulioa hilo, mnalitenda hata hivyo, maana linapendwa na watu wengi. Ibilisi daima amekuwa na jambo linalopendwa na watu wengi. Imekuwa hivyo daima,

tangu mwanzo, “mfano wa dini.” Kaini alikuwa na jambo lile lile. Hii hapa roho yake ikitenda kazi moja kwa moja humu ndani, kupitia kwa mpinga Kristo; na huyu hapa Habili anakuja, aliyeuawa, pia. Hiyo ni kweli. Angalia, basi sasa angalia.

¹⁴⁰ Wanyama hawa wote, kule nyuma, wote waliishia katika mnyama mmoja hapa, ambaye aliitwa “joka jekundu,” Ibilisi.

Sasa hebu tuanzie kwenye aya ya 15 ya sura ya 13.

¹⁴¹ Mnaona sasa ya kwamba *Rumi* ilikuwa—ilikuwa “kiti cha Shetani.” Yule mnyama mwenye vichwa saba na pembe kumi alisimama karibu na yule Mtoto, Mtoto Kristo, apate kumla Yeye mara tu alipozaliwa. Ni nani aliyefanya jambo hilo? Herode, Rumi; daima imekuwa namna hiyo. Tutapata katika Danieli, moja kwa moja, kama tukiwa na wakati wa kutosha, na Bwana akitusaidia, nasi tutaona.

¹⁴² Kama vile kila mahali katika Maandiko, kutoka mwanzo wa Mataifa, moja kwa moja huko nyuma kutoka Mwanzo, ninaweza kuthibitisha kwamba Babiloni ilianza katika Mwanzo na inashia katika Ufunuo. Ilianzia kule nyuma pamoja na Nimrodi, mwana wa Hamu, kupitia kwenye ibada za sanamu, kuingiza sanamu ndani, kuabudu sanamu. Na imekuja moja kwa moja, na, ni janja sana katika siku za mwisho hata inachukua jina la Ukristo, na, hata hivyo, ni ibada za sanamu!

¹⁴³ Si Paulo mkuu, katika Wathesalonike wa Pili, alisema? Hebu tulisome tu, kabla hatujaenda mbele zaidi. Wathesalonike wa Pili, sura ya pili, na tuone kile Paulo alichosema hapa. Hata aliliona hilo katika Roho, kabla hata halijafikia siku tunayoishi.

¹⁴⁴ Vema, jamani, jinsi siku tunaoyoishi, giza tunaloishi ndani yake, huku wanaume na wanawake wakipapasa-papasa hapa katika giza la upagani na hata wao hawajui jambo hilo. Msiba—msiba huo! Jinsi siku ambayo. . .

¹⁴⁵ Paulo alisema, “Siku hiyo haipaswi kuja, usipokuja ule ukengeufu kwanza, akafunuliwa yule mtu wa kuasi.” Sasa angalia, yeye anamtangaza kuwa ni mtu. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Paulo alisema, “Yeye alikuwa mtu wa kuasi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu, hivi kwamba anaabudiwa kama Mungu.” Mtu fulani anayeabudiwa kama Mungu; mtu ambaye angewekwa hapa kama namna ya ibada. Kisha akasema, “Siku hiyo isingekuja usipokuja kwanza ule ukengeufu.” Ni kitu gani? Hali ya uvuguvugu wa kanisa. Vema.

¹⁴⁶ Sikilizeni. Hebu niwasomee, tafadhalini, Wathesalonike wa Pili. Vema. Ninaweza kupata mahali penyewe sasa, kwanza, ili kwamba haitatubidi kusoma mengi sana. “Mtu awaye yote asiwadanganye,” aya ya 3, Wathesalonike wa Pili, sura ya 2.

Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; (Wakati

wa Kanisa la Laodikia sasa)... *akafunuliwa yule mtu (m-t-u, umoja)... mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; (badala ya, badala ya Mwana wa Mungu), mwana wa uharibifu;*

Yule anayepinga, (yeye mwenyewe) na kujiinua nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu, hivi kwamba anaabudiwa kama Mungu; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu. (Akikubali maungamo!)

¹⁴⁷ Usiniambie, rafiki yangu Mkatoliki! [Ndugu Branham anagonga mimbara mara nne—Mh.] Jinsi mnavyosema hakuna kuoa mara mbili; kanisa Katoliki linazungumza juu ya kuoa mara moja.” Kama huna pesa yo yote, hiyo ni sawa. Lakini hebu nikwambie, papa hapa katika watu wangu mwenyewe; kijana mwanamke akiketi moja kwa moja hapa, mama fulani akiketi hapa, na baba, pia; na mwanamke mwingine hapa pamoja na mvulana huyu mdogo. Huyu msichana aliolewa na kijana Mprotestanti; wakaachana wakaenda zao. Kwa hiyo basi, muda si muda, msichana huyo alikuwa aolewe na mvulana Mkatoliki; naye msichana ilimbidi kwenda huko na kulipa pesa nyingi sana, kisha akarudi, na, “Yeye hakuwa ameolewa na mvulana huyu Mprotestanti, kwanza.” Huyu hapa Howard, watu wangu mwenyewe.

¹⁴⁸ Vema, moja kwa moja hapa... Sitalitaja hilo jina. Yeye ana—ana binti, naye huyo binti ana umri wa kama miaka ishirini na sita. Mumewe, alimwacha huko Milltown, kisha akatoroka akaolewa na Mkatoliki. Nao sasa wakasema, “Huyo mwanamume hana budi kutoka kanisani.” Kwa hiyo wakalipa pesa nyingi sana, karudi na “kumbadilisha awe bikira tena,” na kumfanya aolewe na mtu huyu. Upuzi mtupu! Kumbadilisha awe bikira tena? Yeye ameolewa, mbele za Mungu, na anaishi katika uzinzi. Hiyo ni kweli kabisa. Hilo ni BWANA ASEMA HIVI, pia. Kweli.

¹⁴⁹ Ni aibu jinsi gani! “Lipa pesa nyingi humo.” Hiyo ndiyo sababu makanisa haya yote makubwa na mashule yanajengwa. Ni kwa njia hiyo. Ulimwengu mzima... Hamjui jambo hilo, hapa Marekani. Mnapaswa kunifuata kwenye nchi za ng'ambo, wakati mmoja, nanyi mtaona. Naam, bwana. Unaenda kule, ndugu, ambako wao wana mamlaka zaidi.

¹⁵⁰ Naweza kuwaleteeni picha, ya kweli, Ndugu Kopp ndiyo kwanza aipige, kisha akanitumia, ya mhubiri wa Kiprotestanti, mhubiri aliyejazwa na Roho Mtakatifu, amelala barabarani, amevimba karibu ukubwa *huu*, yeye na mkewe, na msichana mdogo, wamevimba namna hiyo; kwa maana wao walimhubiri Yesu Kristo, nguvu za kufufuka, na watu wangepokea kuokoka na kumpokea Roho Mtakatifu. Wao waliwaua kinyaua barabarani,

na wasingekubali wazikwe, na kuwatemea mate, kwa siku baada ya siku. Hiyo ni kweli.

¹⁵¹ Moja kwa moja kule ambako ilimbidi Ndugu Osborn kulindwa, kwa bunduki, wapate kuwaondoa. Wao walishuka wakaenda kule, na mmoja...kundi la makasisi waliungana na kumuua huyu kijana mwanamume. Naye mkewe ndiyo kwanza apate mtoto mchanga. Nao wakapitia mtaani namna hiyo, huku wana wa—wa—walizi wakimpeleka kaburini, wapate kumzika. Naye huyu mama akitembea, huku mtoto mchanga, analia, nyuma ya mumewe aliyekufa. Nao watu wakachungulia dirishani, watu wenye moyo msafi, wakasema, “Kama hivyo ndivyo kanisa Katoliki linavyoona, tunalikataa.” Nao wakafuatwa, na maelfu, kwenye maandamano barabarani. Ndugu Osborn alikuwa na ufufuo kule, mpaka wasingeweza kumfukuza nchini. Kulikuweko na watu wengi kupita kiasi. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁵² Loo, unafiki huo! Najua ni picha mbaya. Ketini kimya tu, enyi marafiki Wakatoliki, tutasugua upande ule mwingine, katika dakika chache. Vema. Angalia.

¹⁵³ Sasa tutashuka tuje, angalieni, mbele kidogo. Hebu niwaambie jambo hili. Labda naweza kuwa na wakati, nina dakika thelathini bado. Angalieni kwa makini. Sasa hebu turudi nyuma, kila msomaji, niani mwenu tu, kwa dakika moja, tupate picha ya mawazo. Wakati...

¹⁵⁴ Kila mwamini wa Kiothodoksi hapa anajua ya kwamba utawala wa Mataifa ulianza na Mfalme Nebkadreza. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kila mwamini wa Kiothodoksi anajua jambo hilo. Naye Mfalme Nebkadreza alikuwa na ono, ndipo Danieli akampa tafsiri. Sivyo? [“Amina.”] Nalo lilikuwa ni kichwa cha dhahabu, ambacho kilikuwa ule wa Kibabiloni; ya pili ilikuwa ya Waamedia na Waajemi; iliofuata ilikuwa ni dola ya Kiyunani; kisha Dola ya Kirumi. Ndipo mwishoni mwa Dola ya Kirumi, Yesu Kristo alikuwa Mwamba uliokatwa kutoka mlimani, bila kazi ya mikonu, uliofingirika na kuivunja-vunja ile sanamu (sivyo?), na kuijaza nchi. [“Amina.”] Mtu ye yote anajua jambo hilo. Mwamini ye yote anajua jambo hilo.

¹⁵⁵ Na jinsi ambavyo, katika siku za mwisho, wakati wao walipovunjika wakawa falme hizi nyingi mbalimbali, na kadhalika, hata kwenye vidole vya miguu, kulikuweko na chuma na udongo. Nazo maana yake, nabii alisema, “Na kama vile ulivyoona chuma na udongo wa matope havitachanganyika, wala hawa hawatashikamana.” Bali watazichanganya hizo mbegu, kujaribu...Kwa maneno mengine, wataoana, wakijaribu kuwalea watoto wao na kuvunja, kujitwalia mamlaka, namna hiyo. Nanyi mnajua jambo

hilo ni kweli. Lakini, lina nguvu, nanyi watu mkijitolea kwake, “Loo,” kasema, “ni zuri sana.”

¹⁵⁶ Mwangalie huyu Stevenson, sijui jina lake ni nani, huku. Sasa nini hii yake...huku. Jina lake ni nani? Ninasahau tu... Jamaa huyu hapa anayesababisha mzozo huu wote hapa. [Kusanyiko linatoa jina—Mh.] Naam. Loo, jamani!

¹⁵⁷ Marekani hii imeoza hata shinani. Naam, bwana. Ninaweza kuwathibitishieni wakati ule ule hasa... Mwanamke huyu hapa, kule nyuma katika Ufunuo 12, wakati...Mtoto wake Mwanamume alinyakuliwa apate kuketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, na, wakati ilipotendeka, huyo mwanamke akakimbia jangwani, mahali alipotunzwa kwa siku elfu moja mia mbili na sitini, kufikia ile tarehe ya Plymouth Rock, hasa, ambapo kanisa lilikuja huku kwa ajili ya uhuru wa kuabudu, nalo likajiimarisha huku.

¹⁵⁸ Basi tutaendelea kusoma sasa kwenye sura ya 13 ya Ufunuo hapa, kisha tuangalie hapa kwenye aya ya 15. Halafu, sasa, hebu kidogo, ninataka kurudi nyuma kabla ya mahali hapo, nasi tuone hapa mahali alipokuwa anasimama kando ya bahari. Sasa kama naweza tu kupapata mahali hapo, ambapo, aya ya 11.

Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; (si kutoka—kutoka baharini)... .

¹⁵⁹ “Kutoka katika nchi.” Halafu, wingi na umati wa watu ni bahari, basi hapa ni mahali ambapo hapakuwapo na watu, Marekani.

...naye alikuwa na pembe mbili kama mfano wa mwana-kondoo,...

¹⁶⁰ “Pembe mbili kama mwana-kondoo,” si mwana-kondoo. Ni kitu gani? Ni nyati wetu wa Kimarekani. Hakika. Mnaona, huyo hapo, “pembe mbili kama mwana-kondoo.” Lakini basi alifanya nini? Alikuwa na uhuru wa kuabudu, kwanza; alitenda kama mwana-kondoo, alinena kama mwana-kondoo. Lakini, kumbukeni, hakufanyika kondoo mume aliyekomaa. Alikuwa mwana-kondoo. Nchi hii ina umri wa miaka mia moja na hamsini tu, mwajua, ni mwana-kondoo tu.

...halafu akanena kama joka.

Naye alitumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. (lile joka jekundu) Naye alifanya dunia na wote wakaa juu ya dunia wamsujudie mnyama wa... , ambaye jeraha lake la mauti lilipona. (Angalia!)

Naye—naye afanya ishara kubwa, hata kujifanyia moto kushuka kutoka mbinguni... (Bomu la atomiki, na haidrojeni; taifa stadi, lenye akili, na kadhalika, likiyadanganya mataifa kwa mambo haya.)

¹⁶¹ Marekani hii itafikia wakati ambapo kanisa na taifa vitaungana pamoja. Ndipo Waprotestanti na Wakatoliki watashirikiana, wapate kupigana na ukomunisti. Nao wanatenda yale hasa Mungu aliyosema papa hapaa.

¹⁶² Nanyi Waprotestanti mnaokaa kule, mmelala fofofu, mkisoma gazeti la mapenzi badala ya Biblia yenu! Huko nje, mkizurura mahali fulani, kwenye namna fulani ya karamu, badala ya mkutano wa maombi mahali fulani; mkizozana ninyi kwa ninyi juu ya mambo madogo ya bure yasiyo na faida *ng'o*. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Unapaswa kuwa magotini mahali fulani, kama unajua maana ya Umilele.

¹⁶³ Angalia, wakati, Mfalme Nebukadreza, hapo mwanzo kule nyuma, hapo majira ya Mataifa yalipoanza. Hebu tuona jinsi yalivyoingia. Na jinsi yalivyoingia, utaona yanaishia vile vile. Tunajua ya kwamba kuna mwanzo wa wakati wa neema kwa ajili ya Mataifa, na mwisho wa wakati. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

¹⁶⁴ Sasa angalieni, wakati Mfalme Nebkadreza...wakati Danieli alipopelekwa kule, nabii mwenye akili, wakati Wayahudi wengine wote walikuwa kwa namna fulani wamenyenyekea nao walikuwa wakiwasujudia Warumi... ama Wababiloni. Bali kulikuwako na watu watatu, wanne; watatu (Shadraka, Mishaeli na Abedinego), na Danieli, walioamua miyoni mwao watamtumikia Mungu. Basi walipowatupa akina Shadraka, na kadhalika, kwenye... Naye Danieli alikuwa amekua mtu mashuhuri, na mbele ya Mfalme Nebkadreza na Belteshaza, na kadhalika. Wakati alipokuwa mtu mashuhuri, sasa angalia, Mfalme Nebkadreza alitengeneza sanamu ya dhahabu akaiweka huko kondeni, kisha akasema ya kwamba kila mtu ingempasa kuisujudia sanamu hiyo.

¹⁶⁵ Mlipata kuona kutokua na hatia kwake, hiyo sanamu ilikuwa ni ya nani? Ilikuwa ni ya Danieli, sanamu ya mwanadamu. Hivi yeye hakusema, "roho za miungu," kafiri? Na kama hao walivyo siku hizi, wana watatu ama wanne wao. "Roho za miungu zinaishi ndani yake," ndipo wakatengeneza sanamu ya Danieli. Ndipo akasema, "Wote ambao hawataibudu sanamu ile, watatupwa kwenye tanuru ya moto." Unaona, Danieli hayuko wakati huo. Mnafahamu ninayomaanisha? "Na mtu awaye yote ambaye hataishujudia sanamu ile, anapaswa kukatwa vipande-vipande, ama kutupwa kwenye tundu la simba, ama kuchomwa kwenye tanuru ya moto, ama cho chote kile, adhabu."

¹⁶⁶ Hivyo ndivyo majira ya Mataifa yalivyoanza, kwa namna fulani ya ibada ya kidini ya kipagani, pamoja na mateso kuwafanya wao waisujudie. Nayo Biblia inabashiri yataishia namna ile ile, "Mtu mtakatifu," Yesu Kristo; sanamu Yake, kuiabudu, na kadhalika.

¹⁶⁷ Mnakumbuka, katika kitabu cha wafia imani cha Fox, wao wangeshikilia msalaba wenye sanamu mbele yao, wakamfungia maksai kwenye kila mkono namna hiyo, nao wangesema... Kama usingekana, kuukana Uprotestanti, kisha uwe Mkatoliki na “kuubusu huu msalaba wenye sanamu.” Wao wangempiga maksai mmoja aelekee upande mmoja, na huyo mwingine upande mwingine, halafu wanawarua. Waliwachoma moto. Walifanya kila kitu. Nimekuwa kwenye yale mapango ya kuzikia; ninajua ninalozungumzia. Pia, mnaona, ya kwamba, hilo ni kweli. Nao hao hapo wamelala. Pia angalia jinsi walivyopitia kwenye zile siku za ufa imani kabla ya Martin Luther. Kulingana na Biblia, pia.

¹⁶⁸ Sasa angalia kwa makini tena sasa. Sasa nawatakeni mwangalie kitu kikubwa. Hivi ufalme huo wa Kibabiloni ulivunjikaje? Usiku mmoja walipoenda kule wakachukua vyombo vitakatifu vya Mungu, wakaanza kunywa divai kwavyo; wakaanza kuwa na wakati mzuri wa kustarehe, na kulichukua kundi la wanawake kule nje, masuria, nao walikuwa wakicheza na kulewa na kujitumbuiza. Sivo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wakati huo kukatokea maandiko kwenye ukuta, “*Mene, Mene, Tekeli, Peresi.*” Hiyo ni kweli? [Amina.”] Nao wakaondoka wakawachukua Wakaldayo wao wote, watu wao wenye elimu, washiriki vuguvugu wa kanisa, wala hakuna mmoja wao angaliweza kuyasoma hayo. Hiyo ni kweli.

¹⁶⁹ Bali walikuwa na mtu pale ambaye angeweza kusoma lugha zisizojulikana, haleluya, angeweza kuzifasiri. Mnaona ninalomaanisha? Yeye aliweza kufasiri lugha zisizojulikana. Hivyo ndivyo uliovyoisha.

¹⁷⁰ Hivyo ndivyo unavyoisha sasa, kwa nguvu za Roho Mtakatifu juu ya watu waliojazwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, walio na nguvu na ishara na maajabu. Hilo hapo Kanisa la Kimataifa likiondoka. Hao hapo waliosalia.

¹⁷¹ Hivyo ndivyo ulivyoingia, hivyo ndivyo unavyoondoka, kabisa, kusujudia na kulazimishwa kujiunga na dini ambayo ni nusu kafiri. Naye Mungu akiingia kwenye ile saa muhimu na kuandika katika lugha zisizojulikana, kisha huyo mtu anazifasiri. Yeye aliweza kuzifasiri. Hakujua lugha hiyo; hakuna mwingine aliyejua. Bali alikuwa na Roho Mtakatifu yule yule, aliyemruhusu kuifasiri hiyo, ndiye Roho Mtakatifu yeye yule Kanisani leo.

¹⁷² Mnamwita Huyo “ushupavu wa dini.” Nitakubali wanao kwa wingi. Lakini, ndugu, kuna aliye halisi pale, pia. Hiyo ni kweli, aliye halisi pale, pia. Ibilisi anatupa kila cha kuigiza awezacho, moja kwa moja njiani, kuwavuruga. Na iwapo hufikirii tena juu ya Mungu kwa kuketi chini na kusoma Biblia yako, kisha uombe na kumuuliza Mungu, basi inaonyesha wewe huihurumii sana nafsi yako.

173 Usonge moja kwa moja kule na kusema, “Mungu, sijali ni vyambo vingapi vya kunguru wa kale Wewe umeviweka kule. Ninaona Biblia Yako iliyopo, nami nimekusudia!” Hiyo ni kweli. “Uliniahidi mimi, uzao wa Ibrahimu.”

174 Mungu alikuwa, utalifikia jambo Hilo; bali kama hukuitwa, sijali wewe ni wa kidini namna gani, umekwisha; hivyo tu, huwezi kuja. Hakuna mtu awezaye, isipokuwa alikuwa. Naye hataki kwamba mtu ye yote apotee, bali wengi wenu watapotea kwa sababu hamjali jambo Hilo kabisa.”

175 Nanyi mtaenda hapa karibu na kuona kitu kinachoonekana kidogo kama ushupavu wa dini, kina kivuli kidogo, “Vema, Dak. *Fulani* alisema *kadha na kadha*, na kadhalika.” Halafu mnatembea humu na kumkufuru Roho Mtakatifu, mnajua hiyo ni kweli, na jambo hilo halitasamehewa kamwe.

176 Mtaona katika dakika chache alama ya Ibilisi ni nini, muhuri wa Ibilisi ni—ni nini, alama ya mnyama. “Mtu awaye yote atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu, hatasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.” Angalia kanisa hilo la kwanza, yale waliyofanya. Angalia, juu ya hili, kanisa la pili! Ungeweza kujifungia nje ya Ufalme wa Mungu, ukaingia kwa Ibilisi; ukaingia huko ambako “hakuna msamaha, katika ulimwengu huu, wala ule ujao.” Kweli. Kwa hiyo, iweni waangalifu, tembeeni kwa uchaji. Iweni waangalifu kwa yale mfanyayo, kwa kuwa hamjui kitakachotukia.

177 Naam, tutaona jambo hili sasa likilundikana. Nina dakika ishirini. Nawatakeni mfungue pamoja nami kwenye sura ya 17, Ufunuo, kumalizia kwa dakika chake tu. Sasa tutamalizia. Sikilizeni kwa makini. Someni pamoja nami. Fungueni Biblia zenu na mwe tayari kusoma. Hili linapaswa kukamilisha jambo hilo.

178 Kumbukeni, kuna alama mbili; moja ni ukengeufu, nyingine ni Roho Mtakatifu. Moja ni alama ya Ibilisi.

179 Kumbukeni, nimesema jambo hili, ya kwamba kanisa Katoliki la mwanzoni... Naam, enyi Wakatoliki, ketini kwa uchaji kwa dakika chache. Kanisa Katoliki la mwanzoni lilikuwa na maoni yao juu ya jambo hilo. Wao walikuwa na fundisho la uongo, la ukaristi takatifu, la kula mkate mwembamba badala ya ubatizo wa Roho.

180 Waprotestani wanachukua kupeana mikono, ama kufanya ahadi; wote wawili wamekosea, kulingana na Neno la Mungu. *Hii* ndiyo ramani. Wao wanakuja na kubatiza, “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” wakati hakuna wakati hata mmoja mtu ye yote alipata kubatizwa namna hiyo; jambo ambalo ni la kipagani kabisa, ubatizo wa Kikatoliki. Nao wanakubali jambo hilo, na kusema, “Ninyi Waprotestanti mnakubali ubatizo wetu.”

Nikasema, “Mbona mnafanya jambo hilo?”

¹⁸¹ Kasema, “Kanisa Katoliki lina mamlaka ya kubadilisha Andiko lo lote wanalotaka.”

Nikasema, “Huo ni uongo.”

Yeye akasema, “Mbona mnaukubali basi?”

¹⁸² A-ha, basi mtanyamaza. Si mimi! Siamini jambo hilo. Hili ni Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. Kama watu wanataka kulifuata, itawabidi kwenda peke yao. Sina budi kuwaambia Kweli. Hiyo ni kweli.

¹⁸³ Angalia, ndipo wakaja na hili lingine lote, kanisa, kujiunga na katekismo yao ya kale na mambo hayo yote pale. Ni jambo la kipuzi na upuzi mtupu namna gani! Nalo limezaa mabilioni ya makafiri, na watu baridi wa kawaida . . .

¹⁸⁴ Ni Ibilisi, hapo mwanzo. Nami naweza kuwathibitishia ya kwamba Biblia ilisema hapa, “Ulimwengu mzima ulistaajabia mamlaka ya mnyama huyu, “aliyekuwako, naye hayuko, tena yuko.” Angewezaje kuwa, “alikuwako, hayuko?” Kasema, “Ulimwengu wote ulishangazwa na jambo hilo.

¹⁸⁵ Wakati Urumi wa kipagani ulipofanyika Urumi wa kipapa, haukuisha kamwe. Ule utaratibu wa Urumi uliisha; wakati mfalme mpya anapokuja, yeye anaweka tu utaratibu mpya. Bali inapofikia kwenye Urumi wa kipagani, kupitia kanisa Katoliki, kupitia upapa, hauishi. Kama papa mmoja akifa, wanamweka mwingine; papa mmoja anakufa, wanamweka mwingine. “Mnyama aliyekuwako, naye hayuko, bali yuko; ambaye hayuko, naye bado yuko; ambaye . . . naye ataenda kwenye uharibifu.” ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI, kupitia Maandiko.

¹⁸⁶ Sasa, sikilizeni. “Akaja mmoja . . .” Nyote angalieni sasa, sura ya 17.

Akaja mmoja wa wale malaika saba, wenye vile vitasa saba (hivyo ni vile vitasa vya mwisho, vinavyomwagwa), akanena nami, akisema . . . Njoo huku, nitakuonyesha hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi;

¹⁸⁷ Angalia Ufunuo 12. Huyu alikuwa mwanamke bikira. Alikuwa bibi halisi. Jinsi alivyosimama vizuri!

¹⁸⁸ Bali huyu hapa mmoja anayeitwa malaya, “k-a-h-a-b-a,” linamaanisha nini hii . . . Ni kitu gani hicho? Hebu na tusifu hili . . . ama tulichambue.

¹⁸⁹ Samahani. Ninaenda mbio sana; nikifikiria nina dakika kumi na tano. Nitakaa saa nyingine moja basi, kwa hiyo ketini kimya. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁹⁰ Angalieni. Vema. Angalieni, hebu tulichambue. Yeye ni mwanamke mchafu. Kahaba ni nini? Ninachukia kutamka neno hilo, bali limeandikwa hapa katika Biblia. Ni mwanamke

anayekiri kuwa mwanamke mzuri, na anafanya uzinzi na wanaume wengine. Sasa, kama mwanamke anawakilisha kanisa, basi ni kanisa linalokiri kuwa ni la Kikristo, nalo linafanya uzinzi na vitu vingine. Hiyo ni kweli?

¹⁹¹ “Naye anaketi juu ya maji mengi; wingi na umati wa watu.” Someni ile. . . yapata aya ya 15 nanyi mtaona jambo hilo, mnaona. Ama, ya 17, katika sehemu hiyo. Tatalifikia hivi punde. “Mwanamke anayeketi juu ya maji mengi; yule kahaba.” Ni kitu cha namna gani! Sasa kama tungalikuwa na siku baada ya siku, ningemchukua mwanamke huyo na kumfuatilia kutoka kwa Kaini hata Kuja Kwake Bwana Yesu, na kuwathibitishia yeye alikuwa wa kwanza kulifanya kanisa madhehebu. Yeye ni mama wa madhehebu. Angalia, “Naye mwanamke anayeketi juu ya maji mengi. Juu, akiketi juu ya maji mengi.”

Sasa aya ya 2.

. . . ambaye (w-a-f-a-l-m-e) wafalme wa nchi wamezini naye, nao wakaao katika nchi wamelevywa kwa mvinyo ya uasherati wake.

¹⁹² Kwa maneno mengine, yeye anakiri kuwa kanisa la Kikristo; la hali ya juu, linapendeza. Angalia jinsi alivyovalia, katika dakika chache, akiwa na lulu na dhahabu na mawe. Wanasema, “Ni nani aliye kama yeye?”

¹⁹³ Naye alikuwa na kikombe mkononi mwake, kimejaa “divai ya uasherati wake,” uchafu wake, mafundisho ambayo anawafanya wafalme, loo, kufanya sala fupi tu na “kuwaombea watoke purgatorio,” na mambo haya yote. Jambo ndilo hilo. Haya basi. Hilo ni Neno la Mungu ninalosoma. Angalia, “Kwa hiyo akanichukua katika. . .” Sasa hebu tuone, huenda ukataka ku-. . . Hiyo ni aya ya 3 sasa. Vema.

Kisha akanichukua katika Roho hata jangwani, nikaona mwanamke, aliyeketi juu ya mnyama mweku-. . . (“Mwekundu,” tajiri, kanisa lililo tajiri kuliko yote ulimwenguni.)

¹⁹⁴ Wao wanalia hapa, “Ni nani anayeweza kufanya vita naye?” Kuna mtu mmoja ulimwenguni, mtu mmoja tu ulimwenguni, ulimwenguni kote, aliye na nguvu kama ono la Mfalme Nebkadreza lilivyokuwa. Hivyo vidole vitano vinaingia katika kila. . . Mstari huo mwembamba wa chuma cha Kirumi unaingia katika kila taifa ulimwenguni. Hakuna mtu mwingine ulimwenguni aliye na mamlaka kama aliyo nayo papa wa Rumi. Rais Eisenhower anaweza kuzungumza Marekani, na inakuwa sheria; bali kuna mataifa mengine anayoweza kuzungumzia, na ni bure. Bali utawala wa Kikatoliki unaweza kuzungumzia huko Rumi, na kila taifa litaitikia kwa sauti kuu. Hiyo ni kweli. Huyo hapo. Sasa tutaona mahali alipo, tuone kama huyo ni yeye ama siye, tuone kama yeye ameonyeshwa hapa vizuri. Vema.

...nikaona mwanamke aliyeketi juu ya mnyama mwekundu sana, (tajiri), mwenye kujaa majina ya makufuru,...

¹⁹⁵ Ubatizo wa uongo; uchumi wa uongo; akiwaongoza watu kijinga, akiwaambia wanaweza kuja tu kanisani, waungame, na kadhalika, kufanya “Salamu Maria,” wafanye vitubio. Ujinga! Upuzi! Sioni jinsi watu, watu wenye akili timamu, wangeamini mambo kama hayo.

...mwenye vichwa saba...

¹⁹⁶ Angalia hapo tena, pepo yuyu huyu aliye kila mahali, lile joka jekundu, yule mnyama na kila kitu, ana “vichwa saba; pembe kumi.”

¹⁹⁷ “Na mwanamke huyo,” yule mwanamke, sasa, kanisa hili. Naam, *mnyama* ni “mamlaka” aliyokuwa nayo, kanisa Katoliki la Kirumi, bali mamlaka ya Katoliki ya Kirumi. Lakini, hili hapa kanisa likizungumza sasa.

Naye mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na chukizo, na machafu ya uasherati wake.

¹⁹⁸ Huyo hapo; na kanisa fulani mnalojua. Sivyo? Halina budi kuwa hapo; limeonyeshwa dhahiri. Endelea kusoma tu nasi tutaona yeye ni nani.

Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la SIRI, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.

¹⁹⁹ Vema, Waprotestanti, hapa ndipo mnapofinyiwa. Mtakubali ya kwamba yeye ni kahaba, bali yeye alikuwa ni “MAMA” (wa akina nani, wa wana?) “WA MAKAHABA.” Hao wangekuwa ni *wanawake*. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hayo yangekuwa ni *makanisa* basi. Sivyo? [“Amina.”] Yeye ni kanisa mama basi. Sivyo? [“Amina.”] Martin Luther alitoka wapi? Ukatoliki. Hawa wote walianguliwa wapi? Ukatoliki, wakileta fundisho lile lile lao, nanyi mnalikubali.

²⁰⁰ Naam, mwanamke aliye mchafu sana katika Jeffersonville anaweza kumzaa msichana mzuri, wa kweli, bikira, hiyo ni kweli, naye anaweza kuenenda vizuri akitaka. Vivyo hivyo kanisa la Kiluteri, la Kimethodisti, na la Kibatisti, na la Kipresbiteri, na kadhalika; walienenda vizuri kwa muda kidogo, wakati—wakati waanzilishi wao walikuwa wanawahubiri Injili. Lakini siku hizi wanaenda kwenye sinema, ni dansini, televisheni, wanavuta sigara, wanafanya cho chote kile, (mnajua ni kweli!), wanakaa nyumbani Jumapili. Ni kitu gani? Kwa maana malaya wako anatenda kama mama yake. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni kweli kabisa.

²⁰¹ Sasa hebu tuone ilipo rangi. Biblia ilisema yeye alikuwa “MAMA WA MAKAHABA.” Na kila mtu anajua hiyo ilikuwa Rumi ya kipagani, ama Bibi Rumi ya papa, kanisa Katoliki. Hivi punde, nitawaonyesha, kumweka mahali pake duniani, mahali atakapoketi hasa. Sawa. Mahali alipo na yeye ni nani, Biblia ilisema hivyo. Si mimi; Biblia! Nayo ikasema ya kwamba yeye aliwazaa makanisa binti kadha wanaomfuata. Sawa, sasa, Wamethodisti, na Wabatisti, na Walutheri, na kadhalika, mnaona mahali mnapoishia, “MAMA WA MAKAHABA.” Wao waliishi sawa, bali Nuru ilipoanza kuangaza . . .

²⁰² Ni kama kundi la mende katika wakati wa kiangazi. Washa taa, barabarani ambapo mende anakula gunzi la kale ama kitu kama hicho, wamulike kisha uangalie wakikimbia kujificha upesi wawezavyo.

²⁰³ Unahubiri Injili, ama ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa mengi ya makanisa haya ya kawaida, yasiyomcha Mungu; kisha uwaangalie, “Hatuamini katika kitu kama hicho. Mimi siamini katika . . .” Mbona? Mnajua mlivyo, hapo mwanzo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

²⁰⁴ Sisemi neno dhidi ya kanisa lako; ndugu, mna watu mle walio lulu. Sisemi kitu dhidi ya Wakatoliki. Ninawapenda Wakatoliki jinsi ninavyowapenda watu wa Maskani ya Branham. Si wewe, rafiki, ninayejaribu kukemea. Si ninyi, Methodisti na Batisti, na Maskani ya Branham. Si ninyi ninaowakemea. Ni dhambi mnayomruhusu Ibilisi aiweke juu yenu! Kwa sababu tu ninyi huenda kanisani, mnafikiri mmeokolewa.

Yesu alisema, “Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hataingia kamwe katika Ufalme.” Basi unapoupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Huko ni kulenga moja kwa moja kutoka begani, ndugu, bali huko ni Begani moja kwa moja kutoka katika Biblia. Yesu hakusema kamwe, “Labda ishara hizi zitafuatana na wengine.” Alisema, “Zitafuatana na hao.”

Loo, wanasema, “Sasa, naamini hiyo ilikuwa kwa ajili ya wale mitume. Ninaamini kuna zamu moja tu ya mitume, na hiyo ilikuwa ni kule nyuma hapo mwanzo.”

²⁰⁵ Na somo lile lile tulilokuwa nalo jana usiku, “Yeye alikuwa na nyota saba katika mkono Wake,” na kila nyota ilikuwa itolewe kwa kila wakati wa kanisa iwe Nuru, sawa; kama tu vile kulivyo na mtume *pale*, kuna mtume *pale*, na mtume *pale*, na mtume *pale*; “ambao walikuwa zile Roho saba,” mwanzoni mwa somo letu, “wakisimama mbele za Mungu, wapate kupelekwa kwenye zile Nyakati Saba za Kanisa.”

²⁰⁶ Loo, ndugu, unaweza kutembea hapa na pale ukiwa na fundisho ndogo la Kibatisti ama la Kimethodisti, na ufaulu; bali liangalie, mbele za Biblia, mara mmoja. Hiyo ni kweli. Amina.

Najisikia wa kidini kwa namna fulani sasa hivi. Amina. Naam, bwana. Angalia. Ndugu, haya basi. Linasaga; bali kucharaza kwo kwote, hakukufanyi nini hii zuri . . .

207 Mama, akiketi kule nyuma, alikuwa akinilazimisha kunywa mafuta ya mbarika. Tulikuwa maskini watoto wachanga. Ilitulazimu kula ugali wa mahindi na maharagwe, kila siku kwa juma, na Jumapili, pia. Haidhuru, ilinibidi kunywa dawa nyingi. Jumamosi usiku, daima angenilazimisha kunywa mafuta ya mbarika. Na Jumamosi usiku ningeshikilia pua langu, namna *hii*, sisemi jambo hili kwa kutania. Ningeshikilia pua langu, kisha ningesema, “Mama, nisingeweza kuyanywa. Yananichukiza sana.”

Yeye akasema, “Kama hayakuchukizi, hayakufai kitu.”

208 Vivyo hivyo na Hii. [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake—Mh.] Itakuchochea! Itavifanya viungo vya—vyako vya kusaga chakula mwilini vianze kufanya kazi sawa, ili kwamba upate kula Injili yote.

209 Mlutheri alikuja moja kwa moja na kuhesabiwa haki. Mbona, wao walikuwa tu. . . Wakaunda madhehebu, “Naam, bwana, sisi ndio kanisa!”

210 John Wesley aliona kutakaswa. Akasema, “Ninaona ni tofauti.” Kisha akasema, “Hiyo ni sawa, Luther, bali jambo ndilo hili.” Alikuwa ni nini? Luther alikuwa ndiye nyota ya wakati wake, bali huyu hapa Wesley. Vema.

211 Naam, basi, Waluteri wote walirudi kwenye rafu, kwa maana wao walisahau ile. . . hawaku-. . . Naam, sio wote. . . Ninamaanisha kanisa la Kiluteri. La Kiluteri lingali lina watu wazuri, waliojazwa na Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Lakini sasa wote walirudi kwenye kanisa, katika wakati huo. Vema.

Huyu hapa Wesley anakuja moja kwa moja. Aliwapitisha kwenye wakati wake.

212 Halafu, muda si muda, akaja. . . Baada ya wakati wa Wesley, moja kwa moja ikaja Pentekoste. Nao wakampokea Roho Mtakatifu, wakinena kwa lugha.

213 Jamani, Wamethodisti, na Wanazarayo, na wa Utakatifu, wanasema, “Loo, ni Ibilisi.” Nanyi mnaona walilofanya? Mlimkufuru Roho Mtakatifu. Nanyi mnaona mlipo leo? Hiyo ni kweli. Ninyi, kile mlichofanya hasa. Hakika, mlimkufuru. Nanyi mkakosa kutembea katika Nuru.

214 Na sasa ninyi Wapentekoste mmekuwa wenye uvuguvugu sana, Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, mpaka Mungu anawatema kutoka katika kinywa Chake. Kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

215 Mnasema, “Unaamini katika kunena kwa lugha?” Naam, bwana. “Uliwahi kunena kwa lugha?” Naam, bwana. Namshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hilo. Naam, bwana.

Nimenena kwa lugha, mara nyingi. Nami ninaamini ni Nguvu za Mungu. Naam. Siamini katika ushuhuda wa kwanza, sasa, ni kunena kwa lugha. Lakini ninaamini kuna Nguvu za Mungu zinazokufanya unene katika lugha, ishara na maajabu kufuata. Naam, bwana.

²¹⁶ Halafu Ibilisi aliweka kitisha ndege cha kale kule, mtu fulani ambaye alidhihaki na kutenda kama alikuwa na Roho Mtakatifu. Nanyi nyote Wapilgrim Holiness, na wa Utakatifu, na Wanazarayo, nanyi nyote, mliangalia nyuma na kusema, “Loo, sitaki yo yote ya Hayo. Loo!”

²¹⁷ Loo, rehema! Kama ungalikuwa na Roho Mtakatifu, ama sehemu ya Mungu moyoni mwako, mkatakaswa kama mliyopaswa kuwa, mngalitambua jambo hilo kuwa ni Nguvu za Mungu. Hivi Yesu hakusema, “Kama mngalimjua Musa, mngalinjua na Mimi pia”? Hakika. Kama utakaso ni sehemu ya Roho Mtakatifu ambayo iliwasafisha na kuwatakaswa; kama mngalikuwa na Hiyo, mtatambua Hiyo nyingine yote itakapokuja.

²¹⁸ Mkono *huu* hutambua mkono *huu*. Kichwa *hiki* kinautambua mguu *huu*. Ni sehemu ya mwili.

²¹⁹ Nayo Biblia ilisema kuna karama tisa za kiroho; manabii, waalimu, wainjilisti, na mana-...kadhalika; na—na kufasiri kwa lugha, kunena kwa lugha, Kuponya Kiungu. Atatambua kila sehemu Yake.

²²⁰ Loo, unaganda, “Sitaki kuhusika Nalo kwa cho chote kile.” Whiu! Kunakuwa na joto huku, sivyo? Hiyo ni kweli. Kwa nini? Kwa nini? Mlifanywa madhehebu. Kanisa lenu lilisema jambo hilo, na hiyo ndiyo sababu msingeweza kufanya jambo hilo. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara kadha—Mh.]

²²¹ Bali wengi wenu Wamethodisti mlitoka kisha mkampokea Roho Mtakatifu. Wengi wenu Wabatisti mlitoka na mkapata Roho Mtakatifu. Naam, bwana. Ninyi, na wengi wenu wa Utakatifu mlitoka mkampokea Roho Mtakatifu. Naam. Kwa nini? Hamkujali lilivyosema kanisa. Mlitembea Nuruni. Amina. Hamkujali kile kilichotukia. Mlijua ilikuwa ni ya Bwana, nanyi mkatembea tu ndani Yake.

²²² Kaacha mama mzee—acha mama mzee akae kule nyuma, mama yao wa kale. Yeye anatenda kama mama yake kule nyuma, malaya. Ameunda mahehebu. Hiyo ndiyo kanuni hasa ya mwanzo wa shida, wakati kanisa Katoliki lilipounda madhehebu. Ndipo kanisa la Kiluteri likaunda madhehebu baada yake. Ndipo kanisa la Kimethodisti likaunda madhehebu baada yake. Kisha kanisa la Kibatisti likaunda madhehebu. Na sasa kuna madhehebu mbalimbali mia sita tisini na sita mbalimbali. Na Pentekoste ilifanya jambo lile lile!

223 Utukufu! Kuna nini? Mungu anathibitisha ya kwamba Yeye hayumo katika madhehebu. Yuko katika Roho, Roho Mtakatifu. Haleluya! Haleluya! Naam, bwana.

224 Yeye hajali madhehebu yako ni nini. Ni upuzi. Yameunganishwa na Ukatoliki na yamerudi kwake, na kukaa mle, nawe unapokea alama ile ile liliyo nayo. Hivi yule malaika hakusema, “Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, Nami nitawapokea?” “Msiguse kitu chake kilicho kichafu, Nami nitawapokea,” Roho Mtakatifu akinena.

225 “Na kila aichukuaye ile alama ya mnyama, wala herufi ya jina lake.” Laiti tungalikuwa na wakati wa kuingilia jambo hilo; wakati wangu umekwisha. Herufi ya jina lake ni nini? Uprotestanti. “Na tufanye sanamu yake. Na tuunde madhehebu. “Kanisa letu ni kubwa tu kama kanisa Katoliki.” Wao walichukua mambo haya yote. “Walikuwa na makanisa makubwa, nasi tunayo, pia. Tuna wengi wa tabaka ya mjini, kanisani mwetu, kama vile walivyo nao kwao. “Na tufanye sanamu ya yule mnyama.” Basi Biblia ilikuwa imesema nini, yeye ni “KAHABA,” na hiyo ni “MALAYA,” kupitia madhehebu.

226 Bali kanisa la Mungu aliye hai ni huru. “Yeye ambaye Mwana amemfanya huru ni huru kweli.” Tokeni kwake! Jazweni na Roho wa Mungu.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;
“Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.”

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya wanadamu inakufa kwa woga;
Jazweni na Roho wa Mungu, huku taa zenu
zimetengenezwa na ni safi,
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!
Amina.

227 Jinsi mambo yanavyoendelea! Yeye alisema, katika siku za mwisho, “Msiogope, enyi kundi dogo. Ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa Ufalme,” tukikaa pamoja katika ulimwengu wa Roho.

228 Nawe Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri, ambaye umemcheka mpentekoste. . .

229 Basi, ninasema, Pentekoste inahitaji kupigwa kofi zuri la Injili ya mtindo wa kale, kwa maana wameunda madhehebu. Assemblies of God yenyewe imeingia katika Pen—Pentekoste iliyo kubwa sana, imejiunga na muungamo wa makanisa, ikawa ya kawaida tu na isiyojali vile vile. Na kutendewa vibaya sana nilikowahi kumwona Roho Mtakatifu ametendewa, karibuni, ilikuwa ni mhubiri wa Kipentekoste. Kwa hiyo msifikiri, eti kwa sababu ninyi ni wafuasi wa kanisa la Kipentekoste, mmeokoka.

²³⁰ Umeokolewa tu wakati kweli umebatizwa na Roho wa Mungu, kwa Roho Mtakatifu, ukaungana Naye katika Nguvu za kufufuka Kwake, mkisonga mbele kwa ishara na maajabu, zikimfuata huyo Roho popote Yeye aendako. Ishara zilifuatana na manabii. Ishara zilifuatana na Yesu Kristo. Ishara zilifuatana na mitume. Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao,” mpaka Yeye atakaporudi tena.

“Hilo lilisema hivyo, Ndugu Branham?”

²³¹ “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Nguvu hii na dhihirisho katika kila taifa.” Na bado imepungukiwa na theluthi mbili zake, hata hivyo, ambao hawajasikia Hiyo. “Na ishara hizi zitafuatana na hao.” “Hao!” “Kila taifa!”

²³² Utukufu! Whiu! Loo, jamani! Labda mtafikiri nina kichaa. Ndugu, ninawaambia, ninaipenda hii dini ya mtindo wa kale. Naam, bwana, inakutia nanga katika Kristo!

²³³ Sasa mnaona alama ya mnyama ni nini? Ni alama ya ukengeufu. Ni mtu ambaye ni... anawaza tu, ya kwamba, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa, nami ni mwema tu kama jamaa huyo mwingine. Hivi mimi si mshiriki wa kanisa hili?” Nanyi mnatambua, mahali ambapo madhehebu yako ya kanisa mnayotegemea, yanakotoka? Mnatambua?

²³⁴ Biblia ilisema, “Yeye anayemwabudu yule mnyama, anapokea alama yake, ama herufi ya jina lake,” sasa angalia, “kwenye kipaji cha uso ama mkono,” hiyo ni *maarifa* ama *tendo*. Hiyo haina maana kwamba una mchanjo mkubwa usoni mwako. Si lazima iwe hivyo. Haizungumzii juu ya mambo ya nje. Linazungumza ya kiroho.

²³⁵ Basi mwangalie uone anayojua juu ya Maandiko. Msikilize uone anakoelekea. “Kama mtu ye yote hana Fundisho hili, hamna Nuru ndani yake,” Biblia ilisema. Mnaona? Mnaona? Angalia anakoelekea. Angalia analotenda.

²³⁶ Yeye anasema, “Vema, mimi—mimi ni mshiriki. Mimi ni Mprotestanti. Naam, bwana. Mimi—mimi ni mfuasi wa kanisa *hili* fulani. Naam, bwana.” Na huku Jumapili unaliheshimu kutosha tu kuingia utoke kwenye mvua. Yeye anashuka anaenda, badala ya kwenda kwenye mkutano wa maombi, mtalifunga kanisa, kisha mketi na kuangalia televisheni. Yeye anatoka anaenda hapa nje na kunywa na kufanya yasiyofaa, na kutenda kama walimwengu wengine, hata hivyo yeye ni mfuasi wa kanisa. Kumbuka, hiyo ni alama ya dhambi.

²³⁷ Sasa hebu tusome mbele kidogo, upesi, kisha nitafunga. Tumepita wakati. Hebu tusome sasa aya ya 6.

Nikamwona yule mwanamke sasa (kanisa) amelewa kwa damu ya watakatifu...

²³⁸ “Amelewa kwa damu ya watakatifu.” Mwajua, Biblia ilisema, wakati alipoangamizwa, ya kwamba kila mtu mwenye

mwili aliyekufa, juu ya nchi, hatia ilipatikana katika kanisa Katoliki. Hakika, hapo mwanzo.

*...na kwa damu ya mashahidi wa Yesu. Nami...
(Yohana akizungumza sasa) ...Nami nilipomwona
nikastaajabu ajabu kuu.*

²³⁹ Yohana alisema! Sasa hebu tuangalie hapa. Yohana alisema, “Nilimwanguka; yeye alikuwa mrembo sana, kanisa kubwa zuri. Alikuwa na kundi zima la makanisa yaliyozaliwa kutokana naye, ‘mama wa makahaba.’ Nami nikaangalia kule ng’ambo, na basi mwanamke huyo angewezae... Yeye alikuwa akitoa fundisho hilo la uongo, akiwafanya wafalme wote na watu wakuu kulewa kwalo. Na hapa binti zake wanafanya jambo lile lile. Lakini, nilimwanguka; alikuwa na sura nzuri sana!”

²⁴⁰ Mahali pamoja katika Maandiko palisema, “Ninaketi kama malkia nami sina haja na kitu.” Mnaona?

²⁴¹ Kisha yeye, Yohana, akasema, “Nilistaajabu. Nilimwanguka, na nikamwanguka kwa ajabu kuu. Nikastaajabu.”

*Na yule malaika akaniambia, Kwani kustaajabu?
Nitakuambia... Nitakuambia siri ya mwanamke huyu,
na... mnyama huyu amchukuaye, mwenye... vichwa
saba na zile pembe kumi.*

²⁴² Sasa hebu tuone kama tulikuwa sahihi. Kama tumeupata Ukatoliki vizuri, basi mnajua Uprotestanti unaufuata. Kwa hiyo mna... Ninyi, mna akili ya kutosha kujua jambo hilo, mnaona. Angalia.

*Yule mnyama ambaye uliyemwona alikuwako,...
hayuko, naye yuko...*

²⁴³ “Yule mnyama.” Sasa angalia. Sasa utaona hapa, lilisema ni wafalme wangapi waliokuwako; jinsi walivyoanguka, mmoja hana budi kujua.

...yuko tayari kupanda kutoka kuzimu...

²⁴⁴ Si kwenye Biblia! Yalifanywa kutoka katika kundi la ushirikina. Hakuna msingi wake. Unapata wapi “purgatorio”? Unapata wapi hii “hakuna nyama,” na “kasisi kutoa,” na mambo haya mengine yote wanayofanya, “maungamo”? Unapata wapi hayo? Hakuna mahali po pote unapoweza kuyapata. Yalitoka kuzimu. Biblia ilisema hivyo. Yalitoka, yule mnyama, zile nguvu, lile fundisho alilokuwa nalo, “Yalitoka kuzimu.”

...kisha anakwenda kwenye uharibifu...

²⁴⁵ “Uharibifu” ni wapi? Kuzimu. Anarudi moja kwa moja alikotoka.

*...Na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa
majina yao katika kitabu... tangu kuwekwa misingi ya*

*ulimwengu, watastaajabu wamwonapo yule mnyama,
ya kwamba alikuwako, . . . hayuko, naye atakuwako.*

246 Naam, makanisa ya Kiprotestanti yanasema, “Vema, hilo linaweze kanaje, wakati wanaposema, ‘Ninamwamini Yesu Kristo. Yeye ni Mwokozi wangu?’” Ibilisi anaamini, pia, ndugu.

247 Haina budi kuwa ni wongofu, Kuzaliwa upya, kuzaliwa mara ya pili. Na wakati unapozaliwa mara ya pili, jina lako linaandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

248 Unasema, “Nashangaa kila mara. Vema, vipi, mimi si ni mzuri kama mtu mwingine ye yote? Mimi si ni mzuri kama kundi lenu mabaradhuri watakatifu wanaojifingirisha? Nina akili vile vile. Ninazo ndani. . . Nina madigrii. Nimetoka chuoni. Nimetoka kwenye jamaa bora. Watu wangu walikuwa wafuasi wa kanisa, walionitangulia. Si mimi ni bora tu kama mlivyo ninyi?”

249 Ilisema, “Ulimwengu wote,” Waprotestanti na hao wote, “walistaajabu,” wote isipokuwa wale ambao majina yao yaliandikwa katika kile Kitabu.

250 Kwa nini majina yaliandikwa? Wao ni Mzao wa Ibrahimu, “nao ni warithi kulingana na ahadi, waliteuliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Hiyo ndiyo sababu wao hawastaajabu. Angalieni hapa, sasa angalieni kile alichosema. Angalieni haya katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

Hapa ndipo penye akili ambazo zina hekima.

251 Sasa nataka kuwauliza jambo fulani. Je, hekima ni moja ya karama za Roho Mtakatifu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Biblia, Wakorintho wa Kwanza 12, inafundisha ya kwamba karama na kila kitu kanisani, ni hekima, hebu tuone, moja ya karama? [“Amina.”] Vema, ungewezaje kusema hakuna kunena kwa lugha basi? Unasemaje hakuna kufasiri lugha? Ungewezaje kusema, hakuna kuponya Kiungu? Kwa kuwa mwili ule ule. . . Kama mimi ni mwili fulani, nina mkono upande *huu*, na mkono upande *huu*, na mguu *pale*; unawezaje kusema kwamba mkono si mguu? Hivi hukusikia alivyosema Paulo?

252 Sasa angalia, yeye anauzungumzia katika siku za mwisho, moja kwa moja ule Mwili, kasema, “Hapa ni kwa yule aliye na hekima.” Loo, ninapenda jambo hili. Lo, jamani! Hili hapa ndilo litakalowashtusha. Sikilizeni jambo hili. Sawa. “Hapa ndipo penye akili zenye hekima. Kama karama hizo za Roho Mtakatifu haziji kwa nyakati zote, kwa nini akasema haya kwa ajili ya siku za mwisho basi? Kama hakutakuwako na karama kanisani, katika siku za mwisho, kwa nini Yeye alielekeza haya kwenye siku za mwisho basi? “Hapa ni kwa mtu aliye na hekima.”

*. . . Vile vichwa saba ni milima saba anayokalia
mwanamke huyo.*

253 Ni vilima vingapi? Ni miji mingapi ulimwenguni, hata hivyo, ambayo kanisa fulani hukalia vilima saba? Mmoja peke yake. Uko wapi? Mji wa Vatican huko Rumi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Biblia ilisema ya kwamba kahaba huyu wa kuchukiza aliyeufanya ulimwengu wote kufanya uzinzi, na akazaa kundi la binti wadogo kufundisha karibu kitu kile kile alichofundisha; hawakuwa wabaya kama yeye, bali wao walikuwa makahaba. Aliwafundisha jambo lile lile. Kasema, "Mwanzo wake itakuwa ni mwanamke," ama kanisa, "limekalia vilima saba" katika Rumi. Nimeangalia kila mahali ulimwenguni; niambieni mahali lilipo, "kanisa lililokalia vilima saba." Sasa ninasoma jambo hili kutoka katika Biblia.

Navyo ni wafalme saba. Watano wamekwisha kuanguka, . . .

254 Kama tungechukua historia, na turudi moja kwa moja nyuma na kuonyesha jambo hilo, ambapo hao wafalme walikwisha anguka, huko Rumi, tangu ufalme wa Babiloni.

. . .mmoja yupo (Nero), na mwingine hajaja bado. Naye . . . imempasa kukaa muda mchache (kama miezi sita) atakapokuja.

255 "Na yule mnyama . . ." Loo! Angalia jambo hili. Sasa ile nguvu itapachukua mahali pa mpagani.

Na yule mnyama aliyekuwako naye hayuko, . . . ndiye wa nane, (sasa angalia) naye ni mmoja wa wale saba, . . .

256 Mnajua jinsi alivyokuwa mfalme mbaya. Alikuwa na . . . Alimfungia mamaye kwenye mti mmoja wa farasi na kumkokota mitaani, kisha akauteketeza mji kwa moto, na kucheza zeze kilimani. Huyu ni roho wa namna ile ile anayelitawala kanisa linalokalia mahali pa kipagani. "Wa nane, ambaye ni mmoja wa wale saba. Naye yupo, tena hayupo; naye yupo, tena hayupo; naye yupo, tena hayupo," na kuendelea.

. . . naye anaenda kwenye uharibifu.

257 Moja kwa moja mpaka wakati wa kule Kuja kwa Bwana, naye anatupwa katika kuzimu.

Na zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, ambao hawajapokea ufalme bado, lakini wapokea mamlaka kama wafalme muda wa saa moja pamoja na yule mnyama.

258 Loo, laiti tungalikuwa na . . . "Hawajapokea mamlaka bado." Hao si wafalme. Hawakuwa . . . Hawawezi kuwa. Hizo pembe hazikuwa na taji. "Walipokea mamlaka ya wafalme." Ni kitu gani? Watawala wa mabavu; si wafalme waliotiwa taji. Watawala wa mabavu! Loo, jamani!

259 Naam, loo, ninaposoma jambo hili, wakati mwingine moyo wangu huruka kwa furaha, vema, ninapofikiria juu ya vile tunavyoishi hapa katika siku za mwisho.

Na zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, ambao hawajapokea ufalme bado, lakini wapokea mamlaka kama wafalme muda wa saa moja pamoja na yule mnyama.

Hawa wana shauri moja, nao wampa yule mnyama nguvu zao na mamlaka yao.

Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo, na Mwana-Kondoo atawashinda, . . .

260 Hapo vyaja Vita vya Har-magedoni; tayari kwa ajili ya ile Milki ya Miaka Elfu.

. . .kwa maana Yeye ni Bwana wa mabwana, na Mfalme wa wafalme; . . . (usishtuke) . . . na hao walio pamoja naye ndio walioitwa, na wateule, . . .

261 Si wewe; Yeye amekuchagua. Una Roho Mtakatifu, unapaswa kupiga makelele ya ushindi. Mungu alikuchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kama huwezi kuiona Nuru ya Injili, ni kwa sababu wewe—wewe ni kipofu tu.

. . .wateule, na waaminifu.

Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa . . .makutano na mataifa na lugha.

262 Kwa maneno mengine, mwanamke huyu anayeketi hapa, kanisa, atatoa fundisho lake kwa kila watu, jamaa, na lugha. Huyu hapo. Yeye alikuwa na utawala juu yao. Anakaa juu yao, mamlaka yanayowatawala. Yeye anakalia vilima saba, amevaa nguo nyekundu, amepambwa akiwa tajiri sana kuliko wote ulimwengu. Huyu hapo.

Na zile pembe kumi ulizoziona, na huyo mnyama, hao wata- . . .

263 Angalia sasa, unaingia katika nguvu za ukomunisti.

. . .hao watamchukia yule kahaba, nao watamfanya kuwa mkiwa na uchi, watamla nyama yake, watamtekeleza kabisa kwa moto.

Maana Mungu ametia mioyoni mwao kufanya shauri lake, na kufanya shauri moja, na kumpa yule mnyama ufalme wao hata maneno ya Mungu yatimizwe.

264 Haleluya! “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno la Mungu halitapita kamwe.” Angalia!

. . .mwanamke uliyemwona, . . .

. . .mwanamke uliyemwona, ni mji ule mkubwa, wenye ufalme juu ya wafalme wa nchi.

265 Nionyeshe mji mmoja ulimwenguni ulio na utawala juu ya wafalme wa nchi, na kwa njia yo yote unayotaka, nje ya utawala wa Katoliki huko Rumi, unaokalia vilima saba. Hakuna mji hata

mmoja, wala haujakuweko, na hautakuweko kamwe; nje ya ule Mji Mpya ulioshuka kutoka Mbinguni. Hiyo ni kweli.

266 Naam, hebu kidogo. Nataka kuwaonyesha jambo hili tena, kwa hiyo Bwana na aturehemu na kutubariki pamoja tunaposoma hili. Vema. Angalia hapa sasa, ninasoma sura ya 13. Ninaanzia kwenye aya ya 15.

Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu . . .

267 Hiyo ni Marekani, tuliyoona ikiinuka, mnaona, sanamu.

. . .hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote ambao wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe. (Huko ni kule kupiga marufuku.)

Naye aliwafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso za . . .zao;

Tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake.

268 Sasa angalia, sasa, kwa makini sasa, kwa makini sana, kabla hatujafunga. Aya ya 18. Sikilizeni.

Hapa ndipo penye hekima.

269 Mnaona Roho Mtakatifu akiwakumbusha waamini katika siku ya mwisho? Kundi hilo dogo pale, akinena, akiliita hilo kundi dogo katika siku hii, “Hapa ni kwake aliye na hekima kanisani. Na afahamu jambo hili.”

. . . Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni hesabu ya kibinadamu (si taifa) kibinadamu. Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita.

270 Na moja kwa moja juu ya Mji wa Vatican . . . Usiniambie sasa; mimi nina *Kanuni za Imani Yetu*, na kadhalika, mnaona. Juu ya Mji wa Vatican, na papa anasimama kama “aliye badala ya Mwana wa Mungu.” Nina marafiki Wakatoliki wanaoketi papa hapa, waliokuwa Wakatoliki, wameketi hapa na wanajua hilo ni kweli. Watu wangu, labda, walionitangulia, walikuwa Wakatoliki, pia. Mnaona?

271 Wao walimwita Mtakatifu Patrick Mkatoliki, naye hakuwa Mkatoliki kamwe. Kasema Joan wa Arc alikuwa mtakatifu; nao makasisi walimchoma moto kama mchawi. Si ajabu Yesu alisema, “Mnayapaka chokaa makaburi ya manabii, nanyi ndinyi mliowaweka mle, enyi kuta zilizopakwa chokaa.” Hiyo ni kweli.

272 Angalia, ni hesabu ya mwanadamu. Na juu ya papa wa Rumi, imeandikwa, “VICARIVS FILII DEI.” Imeandikwa katika herufi za Kirumi. Hebu ziandike wewe mwenyewe, kesho. V,I,C,I,R, loo, ziandike tu, katika herufi za Kirumi, kisha uchore mstari na

kuzijumlisha, uone utakachopata: mia sita sitini na sita. Yeye anakaa wapi? “Juu ya vilima saba.”

²⁷³ Na kutoka kule kukatokea madhehebu ya dini, ambayo yalifundisha mafundisho ya sharti badala ya Biblia. Nao Waprotestanti wakatoka kwake, na wanafanya jambo lile lile wao wanalofanya, maana Hilo lilisema yeye alikuwa “KAHABA,” nao walikuwa “MALAYA.” Wanatoka na ubatizo wa uongo, pamoja na dini ya uongo, na wazo la uongo la Roho Mtakatifu, pamoja na wazo la uongo la kuzimu, na mambo haya yote namna hiyo, nao Waprotestanti wanafuata moja kwa moja hizo nyayo.

Bali itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Njia ya Utukufu hakika mtaipata; (hiyo ni kweli)
... maji, ndiyo Nuru leo,
Mkizikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia;
Nuru za jioni zimekuja,
Ni dhahiri kwamba Mungu na Kristo ni mmoja. (Amina!)

²⁷⁴ Ndugu, ninakwambia, ni Nuru za jioni zinaangaza. Fundisho lile lile la kimitume, ubatizo ule ule wa kimitume, kujazwa kule kule kwa Roho Mtakatifu kwa kimitume, ishara zile zile na maajabu yale yale ya kimitume, zinapenyeza na kuingia kwa Mataifa; kama zilivyofanya kwa Wayahudi, huko nyuma asubuhi na mapema, haya hapa kwenye machweo ya jua.

Kuna watu karibu kila mahali,
Ambao mioyo yao wote inawaka moto
Kwa Moto ulioanguka Pentekoste,
Uliowaosha na kuwafanya safi;
Loo, unawaka sasa ndani ya moyo wangu,
Loo, utukufu kwa Jina Lake!
Nina furaha ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

Walikuwa wamekusanyika kwenye chumba cha juu,
Wote wakiomba katika Jina Lake,
Walibatizwa na Roho Mtakatifu,
Na Nguvu za utumishi zikaja;

Sasa yale aliyowafanyia siku hiyo
 Atakufanyia vile vile,
 Nina furaha sana kwamba naweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

Si u mmoja wao? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Njoo, ndugu yangu, itafute baraka hii
 Itakayousafisha moyo wako na dhambi,
 Itaanzisha mlio wa kengele za shangwe
 Na itaiweka sasa nafsi yako ikiwa inawaka
 moto;
 Loo, inachoma sasa ndani ya moyo wangu,
 Loo, Jina Lake litukuzwe,
 Nina furaha sana kwamba naweza kusema
 mimi ni mmoja wao.

²⁷⁵ Loo, kwa ajili ya Injili hii tukufu!

Inatiririka damu, naam, inatiririka damu,

²⁷⁶ Hesabu gharama! “Kama atanifuata Mimi, na ajikane mwenyewe, achukue msalaba wake (mauti) na anifuata Mimi.”

Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka damu,
 Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
 Kweli,
 Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka damu.

Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa
 Roho Mtakatifu,
 Alikuwa ni Yohana Mbatizaji, lakini alikufa
 kiume;
 Kisha akaja Bwana Yesu, wakamsulubisha,
 Yeye alihubiri ya kwamba Roho angewaokoa
 watu katika dhambi.

Kulikuweko na Petro na Paulo, na mtawa
 Yohana,
 Waliyatoa maisha yao kusudi Injili hii ipate
 kuangaza;
 Walichanganya damu yao, pamoja na manabii
 wa kale,
 Ili kwamba Neno la kweli la Mungu lipate
 kutangazwa kwa uaminifu.

Ndipo wakampiga mawe Stefano, alihubiri
 dhidi ya dhambi,
 Aliwakasirisha sana, wakauponda-ponda
 ubongo wake;
 Bali alikufa katika Roho, akatoa roho yake,
 Ndipo akaenda kujiunga na wengine, jeshi hilo
 litoalo uzima.

Inatiririka damu, naam, inatiririka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
Kweli,

Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka damu.

Nafsi walio chini ya madhabahu, wanalia,
“Hata lini?”

Bwana atakapowaadhibu hao waliofanya
makosa; (kutania, mnaona. Loo, jamani!)

Bali kutakuwako na wengine zaidi watakaotoa
damu ya maisha yao

Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na
mafuriko yake mekundu sana.

Inatiririka damu, naam, inatiririka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inaendelea
kutiririka damu,

Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
Kweli,

Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka damu.

²⁷⁷ Na tugeuke, tupeane mikono sisi kwa sisi sasa.

Inatiririka damu, naam, inatiririka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka damu
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
Kweli,

Injili hii ya Roho Mtakatifu inatiririka damu.

²⁷⁸ Mnampenda Bwana? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]
Bwana awabariki.

²⁷⁹ Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utawabariki wasikilizaji
hawa, na ujalie waende nyumbani wakifurahi. Jalia waje kwenye
Chemchemi iliyojaa Damu, inayotoka kwenye vena za Imanueli.
Jalia waache ukanisa wote wa kale, kisha waje wampokee Roho
Mtakatifu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu awabariki. Usiku mwema. Mungu awe pamoja
nanyi.



ALAMA YA MNYAMA SWA54-0513
(The Mark Of The Beast)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, 13 Mei, 1954, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1994 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org